SportPesa
TZS. 559,183,880
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Majaliwa** asimamisha kazi ofisa tuhuma za ubadhirifu wa fedha

UKURASA 3



**Mbappe asema hana tatizo na Neymar**

UKURASA 21


# Nipashe

Jumamosi Oktoba 9, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580728

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

...ter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




# CCM yaonya polisi unyanyasaji raia

• **Waziri** Maliasili, IGP kupewa jukumu kurekebisha dosari zilizojitokeza... *Endelea ukurasa 2*



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akikata utepe kama ishara ya kuzipokea ndege mbili mpya aina Airbus A220-300, baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume, Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Serikali yapokea ndege mpya kuimarisha ATCL

UKURASA 2

**Bil. 10/- zatumika kuagiza biskuti**

UKURASA 3

**MICHEZO** **SIMBA YAJIFUNGIA KUISOMA GALAXY** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Askari wa Kikosi cha Zimamoto na uokoaji, wakizima moto uliokuwa ukiteketeza mabweni matatu ya kituo cha kulelea watoto yatima cha Huruma Center kinachomilikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Iringa, jana. Chanzo cha moto huo bado hakijajulikana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# CCM yawaonya polisi unyanyasaji raia

**Na Mwandishi Wetu,** KAHAMA

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, ameagiza kukomeshwa mara moja vitendo vya unyanyasaji wa wananchi katika Jimbo la Ushetu, Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga.

Miongoni mwa manyanyaso hayo ni ukamataji wananchi usio na staha hususan kwa wale wanaodaiwa kukutwa na mazao ya misitu ikiwamo mkaa.

Pia amelitaka Jeshi la Polisi wilayani Kahama kuwatazama baadhi ya askari wake wanaodaiwa kuwabambika kesi wananchi kwa madai ya kukamatwa na bangi.

Akizungumza katika mkutano wa kampeni za uchaguzi mdogo wa ubunge wa Jimbo la Ushetu uliofanyika Kijiji cha Iboja juzi, Shaka alisema CCM hataki kusikia aina yoyote ya unyanyasaji dhidi ya wananchi.

"Nimeelezwa na wananchi kuwa moja ya changamoto hapa Ushetu ni maofisa wa TFS (Wakala wa Huduma za Misitu) kuwakamata katika namna ya manyanyaso ikiwamo kuwadhuru na kuwaharibia vifaa vyao kama baiskeli wanazozitumia kusafirisha mkaa.

"Jambo hili sio sawa, kama kuna tatizo, njia bora ya kukabiliana nalo ni kutumia namna sahihi za kisheria, siyo kuwashambulia, kuwaharibia vifaa na wakati mwingine kuwadhuru maungoni," alisema.

Shaka alisema wapo baadhi ya askari polisi wanatumia kisingizio za cha biashara ya bangi kuwakamata wananchi na kuwaweka mahabusu bila kuwafikisha katika vyombo vya sheria.

Alisema kutokana na dosari hizo mbili, atazungumza na wahusika, akiwamo Waziri wa Maliasili na Utalii kwa upande wa tatizo linalohusiana na madai ya mazao ya misitu, pia atazungumza na Mkuu wa Jeshi la Polisi, Simon Sirro, ili hatua zichukuliwe dhidi ya wahusika.

Kuhusu uhaba wa maji, miundombinu na huduma za afya, Shaka alisema serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia Suluhu Hassan imeshatoa mafungu ya fedha katika kila sekta na miongoni mwa wanufaika ni Jimbo la Ushetu na Wilaya ya Kahama kwa ujumla.

"Kwa mfano kuhusu barabara, serikali imetoa Sh. milioni 500 kwa kila jimbo ili kuifanyia ukarabati barabara zake zipitike kwa ufanisi na kuwafungulia wananchi milango ya usafiri na usafirishaji.

"Kuhusu maji, nakuhakikishieni serikali imedhamiria na inatekeleza kwa vitendo kumtua mama ndoo kichwani. Imeshatoa Sh. milioni 400 kukamilisha upembuzi yakinifu kwa ajili ya Jimbo la Ushetu na hiyo ni hatua muhimu kuhakikisha maji yanayotoka Ziwa Victoria yanawafikia wananchi wa Ushetu," alisema.

Mbunge wa Shinyanga Mjini ambaye pia ni Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Vijana, Ajira na Kazi, Patrobas Katambi, alisema serikali inatekeleza kwa vitendo mkakati wa kuwajengea uwezo wananchi wa kushiriki shughuli za kiuchumi.

## Moto wateketeza kituo cha yatima

**Na Francis Godwin,** IRINGA

MOTO mkubwa ambao chanzo chake hakijafahamika umeteketeza bweni la vyumba vinne katika kituo cha kulelea watoto yatima cha Huruma, kinachomilikiwa na kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Iringa.

Mashuhuda wa tukio hilo waliiambia Nipashe jana kuwa moto huo ulianza kuwaka jana majira ya saa 9:00 alasiri.

Amina Sanga mkazi wa Mkwawa, jirani na kilipo kituo hicho, alisema wakati moto huo unaanza kuwaka, alikuwa akipita jirani na kituo hicho na alijua kuna takataka zinachomwa jirani na kituo.

"Sikujua kama ni bweni linawaka moto ila baada ya kusogea ndipo nilibaini kuwa ni moto unawaka na bweni linaungua," alisema.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Manispaa ya Iringa, Tina Mbaga, alisema bweni hilo lilikuwa linatumiwa na watoto 11 lakini wakati moto unawaka ni watoto sita pekee ndio walikuwa wamerejea shuleni na wote wako salama.

Hata hivyo, Diwani wa Mwangata, Galus Lugenge, alisema jitihada kubwa zimefanywa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Iringa kuthibiti moto huo.

Mkuu wa kituo hicho, Mchungaji Joyce Ngandango, alisema hadi jana jioni alipokuwa akizungumza na gazeti hilo, alisema hasara iliyopatikana haijafahamika lakini akasema ni kubwa kwa kuwa mali nyingi zimeteketea kikiwamo chumba cha kuhifadhia vifaa mbalimbali.

Mchungaji Ngandango alisema moto ulianza kuwaka juu ya paa na ulianzia chumba cha watoto wadogo kabisa na ndio waliopiga kelele kuwa moto unawaka japo wote wako salama.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Iringa, Juma Bwire, hakupatikana kuelezea undani wa tukio hilo.

# Serikali yapokea ndege mpya kuimarisha ATCL

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI imepokea ndege zingine mbili mpya aina ya Airbus A220-300 ilizozinunua kwa ajili ya kuiimarisha Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL).

Ndege hizo zilizotengenezwa Canada, zilipokewa kwenye Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume, Zanzibar na kuzinduliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, kwa niaba ya Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

Katika hafla hiyo, Rais Mwinyi aliitaka ATCL kufuata miongozo ya afya katika kujikinga na ugonjwa wa corona ili kuwahakikishia usalama abiria wanaotumia usafiri wa kampuni hiyo.

Alisema idadi ya Watanzania wanaotumia usafiri wa anga ni ndogo, hivyo kuna haja ATCL kuihamasisha jamii kutumia usafiri huo ili kampuni hiyo iwe na gharama nafuu za kiuendeshaji, tofauti na ilivyo sasa.

"Ufanisi wa ndege unategemea juhudi zinazotolewa na taasisi mbalimbali zilizopo katika viwanja vya ndege, hivyo niwasisitize watendaji kufanya kazi kwa ufanisi na kuwa na ushirikiano," aliagiza.

Dk. Mwinyi alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itaendelea ubia wa soko la utalii hasa kwa mashirika ya kati na mashirika ya mbali ili kuimarisha sekta ya utalii na biashara.

Alisema ujio wa ndege hizo mbili ni sehemu ya hatua muhimu za kuiimarisha kampuni hiyo ya ndege kutoa huduma bora kwa wananchi.

Rais alisema lengo la serikali kupitia kampuni hiyo ni kuwa na ndege 16 ifikapo mwaka 2025 na kuwashauri wafanyabiashara kuzitumia ndege za kampuni hiyo.

"Sekta ya anga na usafirishaji ni msingi mkubwa wa kukuza sekta ya utalii na ukuaji wa maendeleo," Dk. Mwinyi alisema.

Aliongeza kuwa serikali zote mbili zimeahidi kuimarisha sekta ya usafiri kwa kujenga miundombinu ya kisasa.

Dk. Mwinyi alisema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuzungumza na wafadhili ili kuimarisha kiwanja cha ndege cha Pemba na kukuza sekta ya uwekezaji na utalii.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisema ndege hizo zinakamilisha idadi ya ndege 11 ambazo zimenunuliwa kwa fedha za wananchi kwa lengo la kuongeza safari ili kutengeneza fursa za kiuchumi.

Akitoa taarifa ya ndege hizo, Mkurugenzi Mtendaji wa ATCL, Ladislaus Matindi, alisema shirika hilo limefanikiwa kufungua vituo 15 ndani ya nchi na vinavyofanya kazi ni 13.

Alisema shirika hilo linafanya safari zake nje ya nchi katika vituo vyake vinane lakini vitatu vilifungwa kutokana na corona na kwamba vinatarajiwa kufunguliwa, ikiwamo China.

Alisema shirika hilo limefanya matengenezo ya ndege zake zote na kuendelea na utoaji wa huduma za abiria na mizigo.

Mkurugenzi huyo alisema ATCL inaendelea kuimarisha mifumo kwa wateja na imeajiri watumishi 644 kutoka 171 wakiwamo marubani 100 kutoka 11, wahandisi 109 kutoka 27, wahudumu wa ndege 121 kutoka 31 na kada zingine 307 kutoka 102 waliokuwapo awali.

Alisema ndege zilizowasili jana zina uwezo wa kubeba abiria 132 kila moja na kuwa angani kwa saa sita bila ya kutua na zina daraja la kwanza kwa abiria 12.

Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, alisema kuwasili kwa ndege hizo kutaiwezesha kampuni kufanya biashara na kusafirisha abiria katika maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya Zanzibar.

Alisema shirika hilo na ndege litakuza sekta za utalii, madini, kilimo na uchumi kwa ujumla.

HABARI KITAIFA

# PM amsimamisha kazi ofisa tuhuma za ubadhirifu fedha

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amemsimamisha kazi Ofisa Mipango wa Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, Omary Chingwile, ili kupisha uchunguzi wa tuhuma za matumizi mabaya ya fedha za ujenzi wa hospitali ya wilaya.

Sambamba na hatua hiyo, Waziri Mkuu ameviagiza vyombo vya ulinzi na usalama, kufanya uchunguzi juu ya tuhuma hizo.

Majaliwa alichukua hatua hiyo juzi, wakati akizungumza na madiwani, watumishi na wananchi wa wilaya, akiwa katika ziara ya kikazi ya kukagua miradi ya maendeleo katika Mkoa wa Lindi.

"Hatuwezi kufanya mchezo na fedha ya serikali. Tunahitaji kila mradi uende vizuri, fedha iliyoletwa lazima itumike kama ilivyokusudiwa," alisema.

Majaliwa alisema Rais Samia Suluhu Hassan, amesisitiza matumizi mazuri ya fedha za umma, ili zikamilishe miradi ya maendeleo ya wananchi na kwamba serikali haitamvumilia mtumishi yeyote anayetumia vibaya fedha za umma.

Pia waziri mkuu alilitaka baraza la madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Liwale, lisimamie vyema fedha za miradi zinazotolewa katika halmashauri hiyo, ikiwa ni pamoja na kubuni vyanzo vipya vya mapato.

"Waheshimiwa madiwani, halmashauri yenu inakusanya mapato hadi asilimia 100, lakini hatujawahi kuona mradi wowote unaotekelezwa na halmashauri na ukawa wa mfano," alisema.

Majaliwa alisema halmashauri hiyo, imekuwa ikiweka makadirio madogo ya makusanyo, ili ionekane inakusanya kwa asilimia kubwa, lakini hata mapato yanayokusanywa, hayakusanywi kwa njia za kielektroniki na kumwagiza Muweka Hazina wa halmashauri hiyo, Gervas Bidogo, kuhakikisha vifaa vyote vya kukusanyia fedha kwa njia ya kielektroniki (POS), vinafanya kazi.

Katika hatua nyingine, waziri mkuu amemuagiza Mkuu wa Wilaya ya Liwale, Judith Nguli, kufuatilia fedha za wakulima wa korosho na ufuta, ambao hawajalipwa na vyama vya ushirika ambavyo vilikusanya mazao yao.

"Nakupongeza mkuu wa wilaya kwa kuchukua hatua ya kumsimamisha kazi Ofisa Ushirika, Ephraim Kipomela, kutokana na upotevu wa fedha za ushirika. Usiishie hapo hakikisha vyombo vyetu vya ulinzi na usalama vinafanya uchunguzi na kubaini fedha hizo zilivyopotea," alisema.

# Mpango ashangaa bil. 10/- kuagiza biskuti nje

**Na Joseph Mwendapole**

MAKAMU wa Rais, Dk. Phillip Mpango, amesema sekta ya viwanda imeshindwa kutengeneza bidhaa zinazokidhi mahitaji ya wananchi, huku akishangazwa na Sh. bilioni 9.8, kutumika kuagiza biskuti nje ya nchi.

Aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati wa kukabidhi tuzo kwa mzalishaji bora wa mwaka, kwenye tuzo za Rais kwa Mzalishaji Bora wa Mwaka (PMAYA) zinazoandaliwa na Shirikisho la Wenye Viwanda Tanzania (CTI).

Mshindi wa jumla kwenye tuzo hizo, ilikuwa kampuni ya kiwanda cha Saruji cha Tanga, mshindi wa pili Kampuni ya Bia ya TBL PLC na mshindi wa tatu kampuni za HANSPAUL.

Dk. Mpango alisema sekta ya viwanda ni muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi na kuboresha maisha ya wananchi, lakini inasikitisha kuona bado inasuasua na kuagiza mawaziri husika kukutana na kuja na majibu ya uhakika.

"Bado tunaagiza bidhaa nyingi mno za viwandani na kwa kuagiza tunapeleka ajira nje ya nchi na kudidimiza viwanda vya ndani. CTI na wizara husika mkae mje na majibu ya namna gani tunaweza kutoka huko. Kuna wenzetu walikuwa huko na wameshatoka, hivyo na ninyi mkutane na msije na majibu mepesi," alisema Dk. Mpango.

Makamu wa Rais alitoa mfano kuwa mwaka jana pekee, zilitumika Sh. bilioni 200 kuagiza bidhaa za vitambaa wakati pamba inazalishwa kwa wingi nchini na Sh bilioni 111, zilitumika kuagiza bidhaa za sabuni.

Alisema Sh. bilioni 93, zilitumika kuagiza mafuta ghafi ya mawese, wakati mawese yanalimwa hapa hapa nchini, Sh. bilioni 33 bia zinazotokana na kimea wakati ngano, mahindi na shairi vinalimwa nchini.

Dk. Mpango alisema sekta ya viwanda ina jukumu la kuhakikisha inapenya zaidi, kwenye soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na ile ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC), ili kuongeza uuzaji wa bidhaa kwenye masoko hayo.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo alisema serikali inaendelea na jitihada za kuboresha mazingira ya biashara na malalamiko mengi ya wafanyabiashara yamepungua.

"Nilipoingia Wizara ya Viwanda (na Biashara) malalamiko yalikuwa mengi sana na CTI na washirika wake walikuwa hawakauki ofisini kwangu wakiwasilisha kero zao, lakini nikuhakikishie kwa sasa malalamiko yamepungua," alisema Prof. Mkumbo.

Alisema kwa zaidi ya miaka minne, mauzo ya nje hayajawahi kupanda kuzidi Sh. bilioni moja, lakini kwa mujibu wa ripoti ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) ya Julai, mwaka huu, mauzo hayo, yameongezeka hadi kufikia Dola za Marekani bilioni 1.1.

Mwenyekiti wa CTI, Paul Makanza, aliipongeza serikali kwa kufanya mageuzi makubwa ya kiuchumi ndani ya muda mfupi iliyokaa madarakani na kuviwezesha viwanda kufanya vizuri.

Alisema licha ya janga la corona, wenye viwanda wameonyesha ujasiri mkubwa kwa kuendelea na shughuli za uzalishaji wa bidhaa, wakati baadhi ya nchi zilishindwa na kufunga baadhi ya kazi zake.

Mkurugenzi Mtendaji wa CRDB, Abdulmajid Nsekela, ambaye benki yake ni mfadhili mkuu wa PMAYA 2020, alisema uimara wa sekta ya fedha unategemea zaidi viwanda.


IDYDC

Iringa Development of Youth,Disabled and Children Care(IDYDC)

**STATEMENT OF RECEIPTS AND PAYMENTS FOR THE YEAR ENDED 31st DECEMBER 2020**

**Receipts and Payments Report**

| | Actual - 2020 | Annual - Budget |
|---|---|---|
| **Receipts** | TZS. | TZS. |
| Opening Balance | 75,433,228.00 | 0.00 |
| Donation- Birgitta funds | 1,912,706.00 | 0.00 |
| IOGT-NTO MOVEMENT (FS) | 104,508,743.00 | 194,762,003.00 |
| Direct Aid Program(DFID/RCA) | 185,455,308.00 | 237,455,043.00 |
| PACT TANZANIA | 186,662,075.00 | 201,705,982.00 |
| Deloitte | 7,950,000.00 | 17,160,000.00 |
| T-Marc Tanzania | 322,628,004.00 | 260,536,400.00 |
| FIFA(FIFA Foundation) | 101,990,680.00 | 130,000,000.00 |
| AKHE | 182,336,722.00 | 152,183,743.00 |
| The foundation for Civil Society(FCS) | 36,407,000.00 | 36,407,000.00 |
| Women Fund Tanzania-Trust | 10,000,000.00 | 10,000,000.00 |
| UNICEF | 30,632,519.00 | 30,632,519.00 |
| IDYDC Hall | 14,535,888.00 | 23,860,000.00 |
| Defferred Local Income | (137,651,487) | 0.00 |
| **Total Receipts** | **1,122,801,386.00** | **1,294,702,690.00** |
| | | |
| **PAYMENTS** | | |
| Alcohol Abuse Prevention project | 99,251,541.00 | 194,762,003.00 |
| DFID/RCA CYLWS Programme Support | 230,023,911.00 | 237,455,043.00 |
| USAID Kizazi Kipya Activities | 185,008,325.00 | 201,705,982.00 |
| USAID Boresha Afya | 9,167,465.00 | 17,160,000.00 |
| USAID Tulonge Afya | 298,146,253.00 | 260,536,400.00 |
| Football for Hope(IFFH) | 51,895,685.00 | 130,000,000.00 |
| Primary School Toilets Construction Project | 182,264,535.00 | 152,183,743.00 |
| FCS PETS in Agriculture Programme | 19,565,178.00 | 36,407,000.00 |
| Tujali Afya Project(WFT) | 9,910,929.00 | 10,000,000.00 |
| IDYDC Afya yetu project(UNICEF) | 15,636,651.00 | 30,632,519.00 |
| Audit fee 2020 | 6,746,040.00 | |
| IDYDC HALL | 15,184,873.00 | 23,860,000.00 |
| **Total Payments** | **1,122,801,386.00** | **1,294,702,690.00** |

Signed by: Zakaria Mwenda (Accountant)

Approved by: Johnnie Nkoma (Executive Director

116502602



## UUZAJI WA MALI

**Mwaliko wa zabuni**

Benki ya Stanbic Tanzania inakukaribisha katika zabuni ya wazi.

- Zabuni zitafunguliwa tarehe 18 Oktoba 2021. Wazabuni au wawakilishi wanakaribishwa kuhudhuria tukio la ufunguzi litakalofanyika saa 9.00 mchana, katika ukumbi mkuu wa mkutano, makao makuu ya benki ya Stanbic, iliyopo katika makutano ya barabara ya Ali Hassan Mwinyi na Kinondoni.
- Zabuni zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji, Stanbic Bank (T) Ltd, S.L.P. 72647, Dar es Salaam. Zabuni zionyeshe wazi kuwa ni kwa ajili ya ununuzi wa gari.
- Zabuni zote ziambatanishwe na ada ya malipo isiyorejeshwa ya shilingi 50,000/=; aidha kwa mfumo wa cheki au fedha iliyowekwa kwenye akaunti ya benki ya Stanbic na risiti iambatanishwe pamoja na nyaraka za zabuni. Jina la akaunti ni Sundry Deposit Suspense ACCOUNT NO. 121000TZS5108001.
- Zabuni ziwasilishwe kwenye sanduku la zabuni lililo kwenye eneo la mapokezi.
- Bidhaa inaweza kukaguliwa Dar es Salaam, tafadhali piga 0746 969 693 au 0767 202 022 kupata taarifa zaidi.
- Mzabuni atapaswa kulipa asilimia 25 baada ya kutangazwa kukubalika kwa zabuni yake na salio linalobakia lilipwe ndani ya siku 7.
- Benki inaweza kukubali zabuni yoyote na haina wajibu wa kuelezea sababu zake.
- Bidhaa itauzwa "kama ilivyo" baada ya mnunuaji kupitia na kuridhishwa na hali ya bidhaa kabla ya kununua.
- Ushindi wa zabuni hautajali ukubwa wake. Benki ndio yenye maamuzi ya mwisho.
- Zabuni ipo wazi kwa jamii yote. Mtu yeyote anaweza kuomba zabuni moja au zaidi.

**Gari:**

| AINA | MODELI | MWAKA WA USAJILI | USAJILI/NAMBA YA USAJILI | MAHALI ILIPO HIFADHIWA | GHARAMA TENGEFU (TZS) |
|---|---|---|---|---|---|
| VOLKSWAGEN | TOUAREG | 2019 | T 260 DTG | BILO STAR MBEZI BEACH YARD | 173,547,251 |

216503202

Stanbic Bank IT CAN BE™

# Vyakula vyaongeza mfumuko wa bei

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MFUMUKO wa chakula kwa mwaka ulioishia Septemba, mwaka huu umeongezeka hadi kufikia asilimia nne kutoka asilimia 3.8 kwa mwaka ulioishia Agosti, mwaka huu, huku bidhaa za vyakula na zisizo za vyakula zikitajwa kuchangia hali hiyo.

Kaimu Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Takwimu za Jamii kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Ruth Minja, alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipozungumza na waandishi wa habari.

"Hili ni badiliko la asilimia 0.2, ikilinganishwa na Kenya na Uganda ambapo mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Septemba, 2021 umeongezeka kwa asilimia 0.3,"alisema Minja.

Alisema hali hiyo imechangiwa na kuongezeka wa bei ya baadhi ya bidhaa za vyakula na visivyo za vyakula.

Minja alisema kuwa baadhi ya bidhaa za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa mfumuko wa bei ni pamoja na unga wa ngano kwa asilimia 6.8, nyama ya ng'ombe kwa asilimia 3.4, maziwa ya unga kwa asilimia 9.2, mayai kwa asilimia tano na viazi mviringo kwa asilimia 4.7.

Pia alitaja baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizochangia kuongezeka kwa mfumuko wa bei ni pamoja na gesi ya kupikia kwa asilimia 2.7, mkaa kwa asilimia 3.5 na huduma ya malazi kwenye nyumba za kulala wageni kwa asilimi 5.7.

Vilevile, alisema mfumuko wa bei wa bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwaka ulioishia Septemba 2021 umeongezeka hadi kufikia asilimia nne kutoka asilimia 3.6 kwa mwaka ulioishia Agosti 2021.

Alifafanua kuwa mfumuko wa bei ambao haujumuishi bidhaa za vyakula na vinywaji baridi kwa mwezi Septemba, 2021 umeongezeka kwa asilimia 4.1 kutoka asilimia nne.

Akizungumzia mfumuko wa bei kwa baadhi ya nchi za Afrika Mashariki kwa mwaka ulioishi mwezi Septemba, 2021, alisema Kenya mfumuko wa bei kwa mwaka Septemba, 2021 umeongezeka kwa asilimia 6.91 kutoka asilimia 6.57 kwa mwaka ulioishia Agosti, 2021.

Kadhalika alisema Uganda mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Septemba, 2021 umeongezeka hadi asilimia 2.2 kutoka asilimia 1.9 kwa mwaka ulioishia Agosti, 2021.

# Ma-DC watwishwa zigo migogoro ya ardhi

**Na Munir Shemweta,** SINGIDA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amewataka wakuu wa wilaya kusimamia na kumaliza migogoro ya ardhi, ikiwamo ile ya mipaka ya vijiji kabla ya kuanza sensa ya watu na makazi, Agosti, mwakani.

Akizungumza wakati ziara ya mawaziri wa kisekta katika Mkoa wa Singida jana, Lukuvi alisema ni aibu kuona hadi sasa kuna migogoro ya ardhi ikwamo ile ya mipaka kati ya kijiji na kijiji, kata kwa kata na wilaya kwa wilaya wakati wanaopaswa kuishughulikia ni wakuu wa wilaya.

"Inakuwaje mkuu wa wilaya aliyepewa nyenzo na Rais anashindwa kushughulikia migogoro ya mipaka katika vijiji au wilaya na wilaya mpaka waziri aje?" alihoji Waziri Lukuvi.

Kwa mujibu wa Lukuvi, wakuu wa wilaya wanapaswa kusimamia na kumaliza migogoro ya ardhi kwenye maeneo ya mipaka ya vijiji ili wakati wa sensa zipatikane takwimu sahihi za idadi ya watu kwenye vijiji.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Binilith Mahenge, alisema ofisi yake itahakikisha inasimamia pamoja na kuifuatilia migogoro yote ya ardhi ikiwamo ile ya mipaka katika wilaya na vijiji ili kumaliza kabisa tatizo hilo.

Akielezea utekelezaji wa uamuzi wa baraza la mawaziri kuhusiana na migogoro ya matumizi ya ardhi kwenye Mkoa wa Singida, Lukuvi alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameelekeza vijiji 11 kati ya 12 ambavyo wananchi wake wanaishi katika maeneo ya hifadhi na yale oevu kuendelea bila kubughudhiwa. Hata hivyo, alisema timu ya wataalamu itabaki mkoani Singida kwa ajili ya kufanya tathmini kujua ukubwa wa maeneo yanayotumiwa na wananchi ukiwamo mtaa mmoja katika mkoa na kusisitiza kuwa Rais ameamua kumega baadhi ya maeneo na kuwapatia wananchi, hivyo hatarajii kuona wakibughudhiwa.

Mkuu wa Wilaya ya Iramba, Suleiman Mwenda, alipongeza hatua iliyochukuliwa na Rais Samia kuamuru wananchi wanaoishi kwenye vijiji vyenye migogoro ya matumizi ya ardhi kubaki. Alisema uamuzi huo utaondoa hofu na taharuki waliyokuwa nayo wakazi wa maeneo hayo kabla ya uamuzi wa serikali.

Katika hatua nyingine, Waziri Lukuvi ameelekeza Mthamini Mkuu wa Serikali kwenda kufanya uhakiki wa fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi wa mradi wa visima vya maji katika mtaa wa Mwankoko katika manispaa ya Singida.

Lukuvi alitoa maelekezo hayo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa baadhi ya wananchi ambao maeneo yao yametwaliwa na serikali kwa ajili ya kupisha ujenzi wa mradi wa visima vya maji katika mtaa wa Mwankoko.

Wananchi hao walidai kuwa uthamini wa fidia kwa wananchi wa eneo hilo halikufanyika kwa uwazi kwa kuwa, kumekuwa na ulipwaji uliotofautiana viwango kwa maeneo yanayolingana.

Mmoja wa wananchi wa kitongoji hicho ambaye eneo lake limetwaliwa, Bibi Asha Mkaku, aliwasilisha malalamiko yake kuwa alilipwa fidia ya sehemu tu ya eneo lake na kumwomba Waziri Lukuvi kusaidia ili aweze kupata haki.

" Naagiza Mthamini Mkuu wa Serikali aje hapa afanye kazi hiyo kujua nani anastahili kulipwa kiasi gani na atakapokuja hapa, yule anayeoona hakutendewa haki aje na nyaraka zake zote" alisema Lukuvi.

Mwankoko ni eneo lenye hifadhi kubwa ya maji chini ya ardhi ambalo visima virefu vimechimbwa kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya maji yanayotimika kwenye mji wa Singida.

Eneo hilo lina ukubwa wa ekari 1,653 zilizotwaliwa na serikali kwa kuwalipa fidia wananchi waliokuwapo eneo hilo lakini baadhi ya wananchi walilalamika kuwa fidia ni ndogo na wengine kudai hawajafanyiwa uthamini.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya DTB, Ravneet Chowdhury (kulia) na Mkuu wa Kitengo cha Biashara cha benki hiyo, Dennis Rauya, wakipokea simu za wateja na kujibu maswali katika kitengo cha huduma kwa wateja, jijini Dar es Salaam juzi, kama sehemu ya maadhimisho ya wiki ya huduma kwa wateja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri awanyooshea kidole watendaji

**Na Mwandshi Wetu,** SINGIDA

WATENDAJI wa mikoa, wilaya, miji na vijiji wametakiwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo kuhakikisha wanasimamia vizuri maeneo ya hifadhi ili kuepusha migogoro kati ya wananchi na serikali.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na watendaji wa Mkoa wa Singida katika kikao cha mawaziri wanane chenye lengo la kutatua migogoro ya ardhi. Kikao hicho kilifanyika katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida.

"Migogoro ya wananchi kuvamia maeneo ya hifadhi inajitokeza wakati watendaji wenye dhamana na walioajiriwa na serikali wapo wanatazama tu mpaka inafikia katika hali hii," alisema.

Masanja alisema mtendaji yeyote atakayesababisha migogoro ya wananchi kwa kutosimamia vizuri eneo lake, hastahili kwenda na kasi ya serikali na ana mpango wa kurudisha nyuma jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan za kutatua migogoro.

"Hakikisheni maeneo yote ya hifadhi ambayo tunayaachia kwa ajili ya wananchi mnayasimamia vizuri ili kumpa nafasi Rais kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi," alisema.

Masanja aliongeza kuwa migogoro hiyo ambayo Rais ameisimamia na kutoa suluhu yake kwa kuiagiza kamati ya mawaziri wanane wa kisekta kuitatua si vyema ikajirudia.

HABARI KITAIFA

# TAMWA yageukia ukatili wa kimtandao

**Na Mary Geofrey**

KATIKA kuelekea kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Kike Duniani, Oktoba 10, mwaka huu, Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) kimewataka wazazi, walezi, wadau, serikali na wanahabari kuchukua hatua za kuondoa aina mpya ya ukatili kwa njia ya mitandao ya kijamii.

Mkurugenzi Mtendaji wa TAMWA, Dk. Rose Reuben, alitoa rai hiyo jana, wakati akizungumza na wanafunzi wa Shule ya Sekondari Mugabe, Dar es Salaam katika tamasha lililohusisha mdahalo, michezo na burudani kuelekea kilele cha siku hiyo.

Maadhimisho hayo ya siku ya mtoto wa kike mwaka huu, yana kauli mbiu ya kimataifa inayosema 'Kizazi cha Digitali, Kizazi Chetu'.

"Kwa hapa nchini matukio kadhaa ya udhalilishaji wa kingono kwa njia ya mtandao yamewahi kuriporiwa, ikiwamo kusambazwa kwa video za ngono zikionyesha watoto wa kike huku mwanamume akifichwa sura," alisema Dk. Reuben.

Alisema aina zingine za ukatili wa kijinsia kwa njia ya mtandao ni kashfa na matamshi ya chuki, jina la akaunti kuibwa na kisha kutumiwa na watu kwa njia za utapeli au kurushwa kwa video za ngono.

"Hali hii imewakuta zaidi watoto wa kike, wenye majina makubwa au maarufu katika jamii." Alisema mkurugenzi huyo na kuongeza kuwa kumekuwa na utamaduni kwa watoto wa kike kurushiwa lugha za udhalilishaji kwa njia ya mtandao, zikiwamo zile zile zinazohusisha baadhi ya maungo yao ya mwili.

Pia alisema picha za watoto wa kike zimekuwa zikisambazwa katika mitandao ya kijamii na kugeuzwa mjadala wa udhalilishaji na kuchangia kuongezeka kwa lugha za udhalilishaji. "Kutokana na kuongezeka kwa matukio haya yanyoendana na ongezeko la matumizi ya mitandao ya kijamii, hatuna budi kupunguza udhalilishaji huu na kuendelea kuhimiza matumizi sahihi, salama na yenye faida," alisema.

Naye mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule hiyo, John Mathias, alisema watoto wamekuwa wakiiba simu za wazazi wao, ili kuangalia picha au video za ngono hali inayoongeza kuwapo kwa matukio ya ukatili kwa jamii.

Naye Mkuu wa Shule hiyo, Mathew Mchome, aliwataka wazazi kusimamia watoto wao katika matumizi sahihi ya mitandao.

"Watoto wanapaswa kwenda na teknolojia, lakini matumizi ya simu yawe ya usimamizi, mtoto asiachiwe simu ni lazima ataitumia kwa mambo yasiyo na maadili kwa jamii," alisema Mchome.

# Msongo mawazo, sonona bado tishio kwa vijana

**Na Francis Godwin,** IRINGA

TATIZO la msongo wa mawazo na sonona kwa vijana chini ya miaka 25 Katika wilaya ya Mufindi mkoani Iringa ni kubwa, hivyo unahitajika msaada wa elimu ya saikolojia ili kuwaepusha kuchukua uamuzi usiofaa kwenye jamii, imeelezwa.

Mwenyekiti wa Chama cha Watoa Huduma za Kisaikolojia Tanzania, Dk. Heriel Mfangavo, aliyasema hayo jana wakati wa mafunzo ya wanahisi kutoka kata za Mdabulo, Ihanu na Luhunga wilayani Mufundi.

Alisema vijana hao ni wadogo, hivyo kama hawatapatiwa tiba ya saikolojia mapema, tatizo hilo wanakuwa nalo na ukubwani wanaweza kufanya majanga makubwa yakiwamo ya mauaji au kujiua.

Alitoa mfano wa mabinti waliopata ujauzito utotoni kwa kubakwa au kurubuniwa kwamba hali hiyo huwa haifutiki kirahisi kwenye akili zao, hivyo lazima elimu ya saikolojia iwapitie mapema ili wasiendelee kuteseka au kutesa watoto.

Mbali na mabinti hao, pia alisema vijana walionyanyasika kwenye familia kwa kutelekezwa na baba mzazi wakiwa wadogo au kupokonywa mali huwa wanakuwa na visasi hadi ukubwani.

Pia alisema kundi lingine linalohitaji msaada wa kisaikolojia ni watu wenye ulemavu ambao baadhi yao wanaishi na msongo wa mawazo na sonona kutokana na vile maumbile au hali waliyo nayo. Dk. Mfungavo pia alisema baadhi ya vyanzo vya jamii kukutwa na msongo wa mawazo ni kukataliwa, kutengwa na unanyapaa wa kiuhusiano.

"Hali duni ya kiuchumi inasababisha watu kupata msongo wa mawazo, hivyo kupitia mafunzo hayo yanayotolewa ni wazi jamii itapunguza tatizo hilo na hata kufanya shughuli kifanisi zaidi .

Kutokana na tatizo hilo, alisema Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi chini ya mradi wa FCWC na YAM kupitia ufadhili wa Finland, mradi huo utanufaisha zaidi ya vijana na watoto 770 wanaotoka katika familia duni katika vijiji 16.

Alisema wanasihi watakaofanya kazi katika mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM), Mufindi mkoani Iringa wanatakiwa kubaini vyanzo vya tatizo la msongo wa mawazo kwa jamii ya watu wenye ulemavu na kuvitafutia ufumbuzi.

Dk. Mfangavo alisema kutokana na ukubwa wa tatizo kwa watu wenye ulamavu, mafunzo hayo yatakuwa na faida kubwa kwao na kuondokana na utegemezi.

Alisema kazi na majukumu 10 ya mnasihi jamii ni kuwezesha wanufaika kubaini mahitaji yao na kufanya malengo yatakayosaidia kutatua matatizo waliyo nayo na kufikia malengo yao.

Dk. Mfungavo alitaja majukumu mengine ambayo wamepewa ni pamoja na kutoa msaada wa kuboresha afya ya akili, hali ya kisaikolojia na kijamii, kusikiliza na kutoa faraja kwa wanufaika wanaopitia wakati mgumu kutokana na matatizo waliyo nayo na kuwezesha kupata msaada unaohitajika na muhimu.




TANGAZO

MKUU WA CHUO CHA KUMBUKUMBU YA MWALIMU NYERERE ANAWAALIKA WANANCHI WOTE KUSHIRIKI KATIKA KONGAMANO LA KUMBUKIZI YA MIAKA 22 YA KIFO CHA BABA WA TAIFA, MWALIMU JULLIUS KAMBARAGE NYERERE.

KONGAMANO HILO LITAFANYIKA TAREHE 12 OKTOBA, 2021 SIKU YA JUMANNE KUANZIA SAA TATU ASUBUHI HADI SAA SABA MCHANA, KATIKA KAMPASI YA CHUO HICHO KIVUKONI JIJINI DAR ES SALAAM.

**MGENI RASMI ATAKUWA WAZIRI MKUU MSTAAFU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA JAJI JOSEPH SINDE WARIOBA**

**MADA KUU NI "MAONO YA MWALIMU NYERERE KATIKA UONGOZI, MAADILI, UMOJA NA AMANI KWA MAENDELEO YA JAMII."**

WATOA MADA SIKU HIYO NI **MHESHIMIWA PHILIP MANGULA** NA **MKURUGENZI MTENDAJI WA TAASISI YA MWALIMU NYERERE JOSEPH BUTIKU.**

***SIYO YA KUKOSA***

***NYOTE MNAKARIBISHWA***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Taifa Stars inaweza kupindua meza ugenini

**PAMOJA** na kufungwa bao 1-0 dhidi ya Benin juzi kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa Dar es Salaam, hakuna shabiki yeyote aliyeponda kiwango cha timu ya taifa ya Tanzania, Taifa Stars.

Wengi walicholalamika ni kukosa mabao ya wazi. Na hilo huwa linatokea kwenye soka, popote pale duniani. Inaitwa siku mbaya ofisini.

Stars ambayo ilikuwa inaongoza kwenye Kundi J, ikiwa kwenye safari ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Kombe la Dunia nchini Qatar mwakani, kwenye makaratasi ilionekana kama ingeweza kushinda mechi hiyo.

Haikuwa hivyo. Nafasi moja tu walioipata Benin waliitumia vema kwa straika anayecheza Ligi Daraja la Kwanza kwenye klabu ya Stade Brestois nchini Ufaransa alifunga bao pekee.

Ukiiangalia mechi hiyo utagundua kuwa kocha wa Benin alicheza kwa kuiheshimu Stars.

Benin walicheza mchezo wa kujilinda zaidi, hasa kipindi cha pili. Ndiyo kipindi ambacho Tanzania ilifanya mashabulizi mfululizo, lakini Benin ikiwa na watu wengi zaidi golini, kiasi cha wakati mwingine mashuti ya wachezaji wa Tanzania waliishia kwenye miili ya wageni hao na kurudi uwanjani.

Kipindi cha kwanza Benin ni kama ilitaka kupata bao la kushtukiza, kwani walionekana kushambulia na kumiliki mpira. Ndiyo kipindi hicho hicho ambacho wachezaji wa Tanzania kina Simon Msuva, Mbwana Samatta na Feisal Salum walikosa mabao ya wazi.

Hii ni kuonyesha wazi kuwa kama Benin wakifunguka Stars wanaweza kutengeneza nafasi nyingi za kufunga mabao.

Kwa jinsi ilivyocheza Stars kwenye mechi dhidi ya Benin, kiufundi ni kwamba ilicheza vizuri zaidi na kutengeneza nafasi nyingi kuliko mechi zote mbili ilizocheza dhidi ya Jamhuri ya Kimokrasi ya Congo na Madagascar. Imetokea bahati mbaya tu imefungwa.

Pamoja na kwamba Benin ni wazuri, lakini ni kwamba wanafungika. Na wangekuwa wamefungwa kama nafasi zingetumiwa vema.

Tunavyoamini ni kwamba Wabenin hawatocheza kama walivyocheza hapa nchini. Watafunguka zaidi. Watacheza soka la kushambulia zaidi. Hiyo itaipa fursa Stars nayo kushambulia na kutengeneza nafasi nyingi za kufunga. Kinachotakiwa ni kutumika tu.

Tunaamini kuwa kama itacheza kama ilivyocheza hapa, au ikiongeza tena nguvu kidogo ina uwezo wa kushinda ugenini.

Hili inawezekana kwani timu ya taifa ya Tanzania imewahi kufanya vema ikiwa ugenini, wakati mwingine kuliko hata nyumbani.

Hata ilivyotoka sare ya bao 1-1 ugenini dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, hakuna Mtanzania yoyote aliyekuwa akitegemea hilo.

Ni mara kadhaa Stars huwaangusha Wabongo nyumbani na kuwashangaza inapocheza ugenini.

Ndiyo maana tunaamini kuwa Stars si tu kwamba ina uwezo wa kuichapa Benin ugenini, lakini hata kumaliza ikiwa kinara wa kundi na kusonga mbele kwenye hatua ya mtoano.

Ni ushindi wa mechi moja tu kwenye michuano hii ya makundi inaweza kuifanya timu kutoka nafasi ya tatu hadi ya kwanza kama ilivokuwa kwa Benin.

Kimahesabu Stars ina nafasi nzuri zaidi ya kuwa kinara wa Kundi J, kama ikishinda mechi dhidi ya Benin. Itafikisha pointi saba kama vinara wao. Halafu itakuwa na mechi ya nyumbani dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, pia ugenini dhidi ya Madagascar ambao mpaka sasa imeshapoteza matumaini kwani haina pointi yoyote ile.


Kama alivyosema nahodha Mbwana Samatta kuwa bado wanapambana na nafasi ipo.

Ni kweli kabisa kuwa Stars jinsi inavyocheza kwa sasa, ina uwezo kabisa wa kupindua meza ugenini dhidi ya Benin kesho.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Barnabas Maro

## Muungwana Lazima Nilonge

# Haki ni jambo linalomstahikia mtu

**HAKI** ni kitu au jambo ambalo mtu anastahiki kupata; utendaji, ufuataji na utumiaji wa sheria na kanuni katika kutimiza jambo; maji, miliki n.k.

Kabla sijaendelea, naomba niwazindue watakaopitia makala yangu kuwa kuna tofauti kati ya "stahiki" na "stahili". Hivyo ni vyema wanaodurusu kutambua tofauti za maneno hayo mawili.

"Stahiki" ni kitendo cha mtu kuwa na haki ya kupata kitu fulani kutokana na ufanisi aliopata. "Stahili" ni kitendo cha mtu kupata adhabu kulingana na jambo baya alilofanya. mfano: "Alistahili adhabu kwa kosa alilofanya." Chondechonde! (Tamko linalomsihi mtu asiache kufanya jambo) wanaohariri safu hii.

"Upendeleo" au "upendeleaji" ni tabia ya kufanya jambo kwa kumili yaani kitendo cha kitu au mtu kuelemea upande mmoja kimawazo au kimatendo; elemea.

"Chuki" ni hisia ya kutopenda kitu au jambo na " chukia" ni kitendo cha mtu kutopenda mtu mwingine au kitu. Poteza mapenzi; kasirika au nuna.

"Chukiza" ni kitendo cha kufanya jambo la kuudhi; kitendo cha kiumbe kufikia kiwango cha kutopendeza kwa wengine kutokana na matendo yake.

Mchezo ni jambo linalofanywa kwa nia ya kuburudisha. Jambo ambalo watu au timu hulifanya kwa kushindana ili kupata mshindi. Kwa hali hiyo, waamuzi wanapaswa kuwa makini sana wanapochezesha michezo ya aina mbali mbali bila upendeleo wowote hata kama timu wazipendazo ndizo zinazofungwa au kuelemewa na timu pinzani.

"Rushwa" ni kitu mtu anachopokea kutoka kwa mwingine au anachotoa kumpa mwingine afanyiwe jambo kwa upendeleo. Kwa majina mengine ni mlungula / mrungura, hongo, chai, chauchau, mvugulio, kilemba.

Timu mbili zinapokuwa uwanjani huwa na wanachama na mashabiki wao wanaotoa hela nyingi ili kujiburudisha na kuzishangilia zinapopambana na zingine.

Wakati naandaa makala yangu, nililazimika kuandika kwa uchache mambo niliyoyaona wakati Yanga ilipokuwa ikipambana na timu ya Geita Gold kwenye uwanja wa Mkapa wilayani Temeke mkoani Dar es Salaam.

Niliyoyaona kwenye mechi ile nilikumbuka moja ya makala niliyoiandika nikiwashauri T.F.F kuwa na Video Assistant Referee (V.A.R.) itakayoweza kuwasaidia waamuzi kuangalia ili kuthibitisha au kusahihisha maamuzi watowayo na kulalamikiwa si na wachezaji tu, bali na watazamaji walio uwanjani, majumbani na kule kunakoitwa vibanda hasara!

Kuna mabao mawili yaliyofungwa na Yanga dhidi ya Geita Gold lakini kwa mshangao mwamuzi aliyakataa yote! Kwanza ni bao zuri lililofungwa dakika ya 47 na Fiston Mayele kwa pasi murua ya Yacouba lakini mshika kibendera akalikataa akidai kuwa mfungaji wa bao lile aliotea kumbe sivyo!

Kama hiyo haikutosha, dakika ya 84 mchezaji Yusuf Athumani akapokea pasi kutoka kwa Heritier Makambo na kufunga bao lakini nalo lilikataliwa na mshika kibendera akidai mfungaji alikwishaotea kabla ya kufunga hivyo likakataliwa kama lile la mwanzo!

Hata kwenye marudio yaliyofanywa na televisheni iliyoonesha mchezo ule hakuna mchezaji yeyote wa Yanga aliyeonekana kuzidi hivyo kuinyima Yanga mabao mawili!

Mpaka nilipokuwa naandaa makala hii, hakukuwa na kauli yoyote iliyotolewa na T.F.F. Kwa maana hiyo, iliridhia makosa ya waamuzi!

Hii ni mara ya pili sasa naishauri T.F.F. inunue V.A.R kwani itasaidia sana kutoa uamuzi sahihi. Kama shida ya hela, nadhani shirikisho la kandanda nchini limepokea na linaendelea kupokea fedha kutoka mashirika mbalimbali nchini. Kwa hiyo linunue V.A.R yake au liombe kwa kampuni zilizo tayari kuisaidia T.F.F. ili kuondokana na kadhia hiyo yaani jambo linalojiri; tukio la kuhuzunisha.

Jambo linaloshangaza ni kuwa wakati marefarii na washika vibendera wanaposhindwa kusimamia kanuni za mchezo uwanjani, uongozi wa T.F.F. wanaokuwa uwanjani huwa wanaangalia tu kwa macho bila kuchukua hatua yoyote dhidi ya waamuzi wanaoshindwa kuchezesha, labda kwa kutokuwa makini, upendeleo au vinginevyo. Wanastahili adhabu.

Mkosa ni mtu anaetenda kinyume cha sheria au taratibu za jamii. Wasimamizi wa jambo lolote hupewa kanuni na taratibu za kusimamia kazi zao. Kama wanashindwa kutimiza wajibu, waoneshwe mlango wa kutokea badala ya kuharibu kanuni za mchezo upendwao na wengi.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784334096**

HABARI KITAIFA

# TARI yaleta neema wakulima wa mchicha

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

BAADHI ya wakulima wa mchicha katika Halmashauri ya Mji wa Kibaha, wameelezea matumaini mapya katika kilimo cha zao hilo kwa kutumia mbegu iliyoboreshwa, kwa ajili ya nafaka na majani, ambayo itawainua kiuchumi.

Wakizungumza baada ya mkutano ulioandaliwa na watafiti kutoka Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) kituo cha Mikocheni, kwa ajili ya kuwapatia elimu ya mbegu mchicha iliyoboreshwa jana mjini hapa, walisema elimu hiyo itawasaidia kuwa na mabadiliko katika kilimo na soko kwa ujumla

Winifrida Mtana, mmoja wa wakulima wa mchicha kutoka katika Kata ya Mbwawa, alisema wanapopata mbegu bora inawahakikishia soko la mchicha wanapopeleka sokoni.

Naye Flora Julius, ambaye tayari ameanza kutumia mbegu hiyo iliyoboreshwa, aliwashukuru watafiti wa TARI, pamoja na maofisa ugani, ambao wamekuwa wakimtembelea mara kwa mara na kumpa ushauri wa kilimo cha mchicha.

Julius alisema endapo wakulima wengine watazingatia elimu waliyopatiwa na kujituma, watavuna na kuuza kwa wingi mchicha na kuuza, Pia watatumia mbegu zitakazopatikana kama nafaka na kutumia na kuuza kujiongezea kipato.

Awali, akitoa elimu ya kilimo cha mchicha kwa kutumia mbegu iliyoboreshwa, kwa ajili ya nafaka ambayo ni Akeri na Poli, mtafiti wa TARI, Dk. Ruth Minja, alisema ziko aina tano za mbegu za mchicha zilizoboreshwa, ambazo ni Madira 1, Madira 2 na Nguruma, ambazo ni kwa ajili ya majani na Poli na Akeri, kwa ajili ya nafaka.

Dk. Minja alisema msingi wa kilimo cha mchicha ni kuwa na mbegu bora na kwamba aina zote tano za mbegu zilizoboreshwa zimepitishwa na serikali na tayari zinapatikana, kwenye maduka ya pembejeo.

"Mchicha unachangia kukua kwa pato la mkulima na kinachotakiwa ni kuzingatia elimu iliyotolewa na kuwatumia wataalamu wa kilimo kupata ushauri muda wote, ili kupata mavuno bora yatakayoinua soko," alisema.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Mji wa Kibaha, Marco Njau, aliwahakikishia wakulima hao upatikanaji wa mbegu hizo pale watakapozihitaji huku akiwasisitiza kutoa taarifa mapema kwa maofisa kilimo walio katika maeneo yao .

Wakulima hao 112 mbali na kunufaika na elimu, pia walipatiwa mbegu bure kutoka kwa watafiti hao, kwa ajili ya kwenda kuanza kilimo cha mchicha kutumia mbegu zilizoboreshwa.



Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu Kampuni ya Umoja Switch, Miriamu Malima (kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya UBX, Seronga Wangwe (kulia) na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya DCB, Godfrey Ndalahwa, wakionyesha mikataba ya makubaliano ya kibiashara kwa taasisi hizo, baada ya kutiliana saini, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbunge ashangaa darasa watoto 200

**Na Mobini Sarya,** TARIME

MBUNGE wa Tarime Mjini, Michael Kembaki, ameshuhudia zaidi ya wanafunzi 200, wakitumia chumba kimoja cha darasa katika shule ya msingi wilayani hapa.

Shule hiyo ina zaidi ya watoto 1,500 na inakabiliwa na uhabawa madarasa, jambo linalowalazimu walimu kuwalundika zaidi ya watoto 200 katika darasa moja.

"Hili jambo halikubaliki yaani darasa limejaa madawati hadi ubaoni mnasema wanafunzi wanakaa humu zaidi ya 190. Kwa nini diwani hamjengi shule nyingine? Mwalimu anafundishaje humu hamuwatendei haki walimu, kwa sababu inatakiwa mwalimu mmoja kwa wastani wa wanafunzi 40," alisema Kembaki.

Alisema jambo hilo atalibeba kama kero na kuliwasilisha katika wizara husika, ili waone namna ya kusaidia shule hiyo, ambayo watoto wengi wa watumishi wa serikali wanasoma hapo na ilikuwa ikitumika kama shule ya mazoezi kwa Chuo cha Ualimu Tarime.

Diwani wa Bomani, ilipo shule hiyo, Mseti Gotora, akijitetea mbele ya mbunge huyo, kuwa wameshindwa kujenga shule nyingine baada ya kuaminishwa na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya kwamba elimu ni bure hakuna sababu ya kuchangisha watu.

"Hata aliyekuwa DC wetu, ambaye amehama naye ametumika kutukwamisha kwa kusema kwamba elimu ni bure, hivyo tukashindwa kuchangisha michango ya kujenga shule. Sababu ya pili ni halmashauri kushindwa kutoa kibali cha kubadili matumizi ya ardhi kwenye eneo, ambalo tulitaka kujenga shule nyigine," alisema Gotora.

Alisema kata hiyo yenye mitaa saba ina shule moja, ambayo iko jirani na makazi ya mkuu wa wilaya, lakini imekuwa na mlundikano wa watoto wengi.

Mwenyekiti wa halmashauri hiyo, Daniel Komote, alisema hajaona kwenye ofisi au halmashauri maombi ya kata hiyo, kutaka kubadilisha matumizi ya ardhi, ili kujenga shule kama alivyodai diwani huyo.

"Kama mnadai kwamba mmeleta maombi halafu halmashauri inachelewa kuwapa kibali, nendeni mkajenge hakuna atakayekuja kuvunja hayo madarasa. Jengeni wakati utaratibu mwingine unafuata, hatuwezi kuvumilia kuona msongomano wa watoto kama huu," alisema Komote.

# Zimamoto walia uhaba vitendea kazi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Zimamoto na Uokoaji, mkoani Shinyanga, linakabiliwa na upungufu wa magari ya kuzimia moto, hali ambayo imekuwa ikiwapa changamoto katika shughuli zao, hasa yanapotokea majanga ya moto.

Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa, Mrakibu George Mrutu, alibainisha hayo jana wakati akizungumza na Nipashe ofisini kwake, mjini hapa.

Alisema jeshi hilo linakabiliwa na upungufu wa magari matatu, kwa maana kwamba mahitaji halisi ni magari manane, lakini yaliyopo ni matano huku matatu yakiwa mabovu, hivyo kutumika mawili tu kwa mkoa mzima.

"Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, mkoani Shinyanga, tunakabiliwa na upungufu wa magari ya kuzimia moto.

Kwa kawaida kila wilaya inapaswa kuwa na magari, lakini kwa Kishapu na Wilaya ya Shinyanga hatuna gari hata moja," alisema Mrutu.

"Manispaa ya Shinyanga tuna magari mawili, linatumika moja lingine bovu, Wilaya ya Kahama tuna magari matatu na linatumika moja tu na suala hili la upungufu wa magari lipo ngazi ya kitaifa wanalifahamu," aliongeza.

Licha ya kukabiliwa na upungufu huo wa magari ya kuzimia moto, alisema wamekuwa wakishirikiana na kampuni, migodi ya madini na Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), kuwapatia magari yao ya zimamoto na kuyatumia, kwenye majanga ya moto.

Katika hatua nyingine, Kamanda Mrutu alitoa wito kwa wananchi wa Mkoa wa Shinyanga, wanapokuwa wanapata majanga ya moto, wawe wanatoa taarifa mapema au kuomba msaada kwa majirani kutoa taarifa kwa jeshi hilo, ili wafike mapema eneo la tukio na kufanya uokozi.

Hivi karibu katika Manispaa ya Shinyanga, kulitokea tukio la nyumba ya mtumishi wa idara ya uhamiaji, mkoani Shinyanga Mwinji Nyombo, aliyokuwa amepanga katika Mtaa wa viwanja vya Mwadui kuteketea kwa moto.

Tukio hilo lilisababisha wananchi kulitupia lawama Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuchelewa kufika eneo la tukio.

Akiwa katika eneo hilo, Ofisa Operesheni wa Zimamoto, mkoani Shinyanga, Isnpekta Edward Lukuba, alisema licha ya kuchelewa kupata taarifa, pia wanakabiliwa na upungufu wa magari, hali iliyowalazimu waazime kwa JWTZ, kambi ya Kizumbi, hivyo kusababisha kuchelewa zaidi kufika eneo la tukio na kukuta mali nyingi zimeshateketea.

# Mchakato wa tuzo za taasisi bora waanza

**Na Halfani Chusi**

MKURUGENZI wa Lavine International Agency Limited, Diana Laizer, ametangaza kuanza rasmi kwa mchakato wa upigaji kura kupata mshindi wa tuzo za Chaguo la Mteja Barani Afrika (Consumer Choice Awards Afrikca), upigaji kura ukipangwa kuanza Oktoba 20 hadi Novemba 11, mwaka huu.

Lavine alibainisha hayo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu utaratibu wa upigaji kura hizo ulivyopangwa kufanyika.

Alisema tuzo zinahusisha kura za wateja, hivyo upigaji wa kura ili kuwapata washindi utafanyika mtandaoni kupitia tovuti yao.

"Kama tulivyosema awali kwamba tuzo hizi zinahusisha kura za wateja, hivyo zoezi la upatikanaji washindi litafanyika mtandaoni kupitia tovuti yetu lakini pia kura zitaanza kupigwa Oktoba 20 hadi Novemba 11.

"Kura za tuzo hizi zinalenga kukuza ubora katika biashara, kampuni na sekta mbalimbali kwenye uchumi kupitia kura za wateja," Lavine alifafanua.

Alisema tuzo hizo zimepanuliwa kutoka kuwa na Tanzania pekee hadi kuwa za Bara la Afrika, akipongeza uungwaji mkono wa Serikali ya Tanzania chini ya Rais Samia Suluhu Hassan kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara.

Pia alizishukuru taasisi kadhaa ambazo zimejitolea kuunga mkono tangu walipoanza safari Juni mwaka huu.

"Nitangulize shukrani zangu za dhati kwa kampuni ambazo zimeungana nasi tangu mwezi wa sita (Juni) mwaka huu, tulipoanza hii safari.

"Ninawashukuru sana ABSA bank, Onono Hotels wenyeji wetu wa leo (jana), Hugo Domingo Limited Revolutions Events, Azania Group limited, Lake Oil limited, Plascon, SGA Security, Ef Outdoor, The Exchange Africa, Insight Security, Delfina Promotions, Wefoot Tanzania Limited," alisema.

# Pori la Mkungunero kuwekwa mpaka mpya

**Na Munir Shemweta,** KONDOA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amesema timu ya wataalamu itapelekwa katika Pori la Akiba la Mkungunero lililopo wilayani Kondoa mkoa wa Dodoma kufanya tathmini na kuweka mipaka upya kwa lengo la kuepusha kuvamiwa.

Waziri Lukuvi alibainisha hayo juzi wilayani Kondoa mkoani Dodoma wakati akizungumza na wakazi wa kijiji cha Bereko akiwa katika ziara ya mawaziri wa kisekta ya kutoa mrejesho wa utatuzi wa migogoro ya matumizi ya ardhi katika vijiji 920.

"Katika Pori la Akiba la Mkungunero tutafanya tathmini upya na kuweka mipaka upya ili wananchi wajue eneo lililohifadhiwa linaanzia wapi na linaishia wapi," alisema Lukuvi.

Kwa mujibu wa Waziri Lukuvi, baada ya kufanyika tathmini upya na mipaka kupimwa hatarajii kuona wananchi wakivamia maeneo ya hifadhi na mapori ya akiba na kueleza kuwa, Rais Samia Suluhu Hassan ameamua kumaliza migogoro ya matumizi ya ardhi katika maeneo mbalimbali nchini.

Akielezea mgogoro wa matumizi ya ardhi eneo la Bereko wilayani Kondoa, alisema, eneo hilo halina mgogoro mkubwa ukilinganisha na maeneo mengine kwa kuwa mgogoro uliopo unaohusisha ekari 17.2 pekee.

Hata hivyo, aliwataka wakazi wa Bereko kujiepusha na tabia ya kuvamia maeneo ya vyanzo vya maji na kubainisha kuwa, serikali haitasita kuwaondoa watakaojenga kandokando ya mito.

Mbunge wa Kondoa ambaye ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia Dk. Ashatu Kijaji, alieleza ujumbe wa mawaziri wanane wa kisekta kuwa wananchi wa eneo la Bereko wana tatizo na msitu wa TFS kwenye Mlima Salanka alioueleza kuwa mipaka yake imekuwa haitabiliki kutokana na kuhamahama.

"Msitu katika Mlima Salanka umekuwa kero na wananchi wanaumizwa, msitu una mipaka isiyotabirika kwa kuwa inahamahama na wakati mwingine inasogezwa kwenye mbaazi," alisema Dk. Ashatu.

Timu ya mawaziri nane ikiongozwa na Lukuvi imemaliza ziara yake kwenye mkoa wa Dodoma katika Wilaya ya Kondoa kwa kutembelea vijiji na mitaa kwenye Pori la akiba la Swagaswaga na vijiji vilivyopo kinga la mita 500 katika pori la akiba la Mkungunero na baadaye kuelekea mkoa wa Manyara.



Mkurugenzi na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Afrika (BOA), Adam Mihayo (kulia), akifanya mazungumzo ya kibiashara na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Jubilee Life Insurance, Helena Mzena, alipotembelea makao makuu ya benki hiyo, jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mara yavuka lengo chanjo UVIKO-19

**Na Robinson Wangaso,** MARA

CHANJO 25,000 za UVIKO-19, zilitolewa na serikali kwa ajili ya Mkoa wa Mara zimeisha na kusababisha idara ya afya mkoani humo kuazima chanjo 10,000 kutoka jijini Mwanza.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Mara, Dk. Juma Mfanga aliyasema hayo jana, alipokuwa akizungumzia suala la chanjo na namna wanavyopambana nalo kwa kutoa elimu kwa wananchi.

Alisema mwitikio huo umetokana na wataalamu wa afya kubadili mbinu na kuamua kuwafuata wananchi katika maeneo ya makazi, biashara, mikusanyiko mbalimbali ikiwamo masoko, minada, misibani, ili kuwapa elimu na wenyewe kukubali kuchanja kwa hiari.

'Mkoa wa Mara kwa awamu ya kwanza ulipatiwa chanjo 25,000 mwanzo watu wachache walijitokeza kuchanja, lakini wa mbinu ya kuanza kuwafuata katika maeneo yao wananchi wameweza kuhamasika na kuchanja mpaka sasa mkoa umeomba chanjo zingine 10,000 kutoka Mkoa wa Mwanza, ili kuendelea kutoa huduma hiyo kwa wananchi wanaohitaji," alisema Dk. Mfanga

Kundi la watu wenye ulemavu mkoani Mara limesema licha ya kuwapo taarifa mbalimbali zisizothibitishwa kitalaamu, zimesababisha idadi ndogo ya watu kujitokeza.

Katibu wa Chama cha Wenye ulemavu wa viungo Tanzania (CHAWATA) mkoani Mara, Leonard Lameck alisema wenye ulemavu kutojitokeza kwa wingi kulisababishwa na kutoshirikishwa kwa kundi hilo hapo awali.

Alisema sababu nyingine ni wengi wao hawana taarifa sahihi kuhusu chanjo hiyo na kwamba mbinu za kuwafuata wananchi sehemu zao zao kazi wao hazijawagusa.

"Watalaamu wanaenda kutoa elimu na chanjo kwa wananchi, bila taarifa na ukiangalia ni wenye ulemavu wachache wanaopatikana katika maeneo hayo," alisema.

Baadhi vijana waliohojiwa juu ya chanjo hiyo, walisema zipo sababu mbalimbali ambazo zilisababisha kutochanja zikiwamo imani potofu, pamoja na upotoshaji unaofanywa na watu katika mitandao mbalimbali ya kijamii.





# RC Mtaka ageukia upandaji wa miti

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, amewataka wakazi wa mkoa huo kuhakikisha kila kaya inafanya maandalizi kwa ajili ya kupanda
miti kuelekea msimu wa mvua za masika ili kulinda mazingira.

Mtaka alitoa agizo hilo jana wakati wa upandaji miti 1,000 katika Shule ya Sekondari ya Bunge iliyoko Kata ya Kikombo jijini Dodoma.

Akiongoza upandaji miti huo, Mtaka alisema umefika wakati kwa Watanzania kujenga tabia ya kupanda miti ili kulinda mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Unakuta kaya haina mti hata mmoja si wa matunda wala kuvuli halafu mkoa wa Dodoma ni moja kati ya mikoa ambayo ina udumavu lakini unaweza kuzunguka hata hapa tuu usikute mti wa matunda hata
mmoja katika kaya," alisema Mtaka

Aidha, alimwagiza Mkuu wa Shule ya Bunge kusimamia miti yote iliyopandwa ili ikue na bila kupoteza hata mmoja huku akisisitiza lazima wanafunzi waifanye kazi hiyo.

Makamu wa Rais wa Ismaili Jamaat, Nizar Bhanji, ambao walitoa miti hiyo 1,000 alisema mpango wa kuunga mkono juhudi za kimaendeleo kwao ni utaratibu wa kawaida.

Bhanji alisema kutoa miti hiyo ni sehemu ya mpango wa mwamko wa kiraia wa jamii ya Waismailia duniani ( The global Ismaili CIVIC Initiative) ambao unalenga kuamsha ari na moyo wa kujitolea kwa jamii yao duniani.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatuma Mganga, alisema miti iliyopandwa shuleni hapo lazima isimamiwe na ikue vizuri ili wakati mwingine wahusika waone faida.

Dk. Mganga alisema wanawake ni watu muhimu katika usafi hivyo kwa kuwa shule hiyo ni ya wasichana basi wajifunze kufanya kazi za kutunza mazingira kuanzia ngazi ya shule.

Hata hivyo, alisema ni aibu kwa mtoto wa kike kushindwa kutunza mazingira kwani hali hiyo inaweza kumfanya kuwa mama ambaye atashindwa kutunza familia yake.

# Wakulima wa zabibu Dodoma wafundishwa mbinu za kisasa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), imeanza kutekeleza mkakati wa kuwafundisha wakulima wa zabibu mkoani Dodoma juu ya teknolojia za kisasa za kulima zao hilo.

Utekelezaji wa mkakati huo umetokana na hatua ya serikali kuliingiza zao la zabibu miongoni kwa mazao ya kimkakati kitaifa.

Akizungumza na Nipashe jana jijini hapa, Mkurugenzi wa TARI Kituo cha Makutupora, Dk. Cornel Massawe, alisema kwa muda mrefu wakulima wa zabibu wamekuwa wakishindwa kupata mavuno mazuri kutokana na matumizi ya teknolojia na mbinu duni.

"Lengo kubwa la mkakati huu ni kuhakikisha wakulima wa zabibu wanaanza kulima kwa kutumia teknolojia na mbinu za kisasa ili waongeze tija katika uzalishaji wao," alisema.

Tofauti na mazao mengine, alisema ulimaji wa zabibu unahitaji umakini mkubwa katika kuzingatia kanuni za uandaaji wa shamba na mashimo, umbali kutoka shina moja hadi lingine, matumizi ya mbolea na mifumo ya umwagiliaji.

"Zabibu huwa zinashambuliwa na baadhi ya magonjwa korofi. Mara nyingi magonjwa ya fangasi ya 'podery mildew' na 'downy mildew, hivyo lengo ni kuwajengea uwezo wakulima juu ya namna bora ya kuyadhibiti magonjwa haya," alisisitiza.

Dk. Massawe alisema uzinduzi wa kituo cha kusambazia teknolojia za kisasa za kilimo uliofanywa na TARI hivi karibuni jijini hapa, utatoa mchango mkubwa katika kusaidia dhima ya kusambaza teknolojia kwa wakulima wa zabibu.

Alisema hadi sasa, TARI Makutupora imeshatambulisha aina 25 za mbegu mbalimbali za zabibu, ikiwa ni pamoja na mbegu za zabibu za kukausha (dry grapes), zabibu za matunda (table grapes) na zabibu za kutengenezea mvinyo (wine grapes).

"Tunaendelea kufanya utafiti mbalimbali kwa lengo la kuzalisha aina nyingi zaidi za zabibu ili kuwapa wakulima fursa ya kulima zaidi na kwa weledi," aliongeza.

Kuhusu mkakati wa uzalishaji mbegu, Dk. Massawe alisema kwa sasa kituo chake kimeshazalisha zaidi ya miche ya mbegu 100,000 na uzalishaji unaendelea.

Pia alisema TARI Makutupora iko kwenye mchakato wa kuagiza takribani aina 13 za mbegu za mvinyo kutoka nchini Afrika Kusini ili kuchochea kasi ya sekta ya uzalishaji wa mvinyo nchini.

Alizitaja aina ya mbegu hizo zinazotarajiwa kuingizwa nchini kuwa ni pamoja na Cabinet Saviugnon, Syrah, Merlot, Durif na Carignan, Chardonnay, Chenin Black, Semillon, Ramsey, R99, R110 na S04.

Kituo cha TARI Makutupora kimeanzishwa kwa ajili ya kufanya utafiti wa kina wa kuzalisha mbegu bora za zabinu pamoja na kuwafundisha wakulima namna ya kulima zao hilo la kibiashara kwa kutumia teknolojia na njia bora.

Tanzania ni nchi ya pili kwa uzalishaji wa mvinyo barani Afrika, ikiwa imetanguliwa na Afrika ya kusini.

Pamoja na rekodi nzuri katika utengenezaji wa mvinyo, mpaka sasa nchi inazalisha mbegu za aina mbili tu za zabinu za mvinyo ambazo ni Makutupora Red na Chenin White, hali inayowanyima wamiliki wa viwanda vya mvinyo fursa ya kuzalisha aina nyingi zaidi za mvinyo.



Katibu wa Bunge ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Bunge, Nenelwa Mwihambi (kulia), akiongoza kikao cha Baraza kilichofanyika katika Ukumbi wa Msekwa, bungeni jijini Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA BUNGE**

# Anwani za makazi zafikia pazuri

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SERIKALI imesema inaendelea na jitihada za kuweka anwani za makazi nchi nzima ili kurahisisha utoaji wa huduma za usafirishaji mizigo na vipeto hasa wakati huu ambapo dunia inakabilina na tatizo la UVIKO-19.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Jim Yonazi, alibainisha hayo juzi jijini hapa alipokuwa akifungua warsha kwa watoa huduma za posta nchini iliyoandaliwa na Mamlaka ya Mawasailiano Tanzania (TCRA).

Dk. Yonaz alisema hadi sasa halmashauri 21 tayari zimefikiwa na huduma ya anwani za makazi huku kazi ya kufikisha na kuunganisha nchi nzima mfumo huo ikiendelea.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kila mtaa, nyumba, njia na barabara zinatambulishwa kwa anwani maalum chini ya utaratibu wa 'postcode', ili kurahisisha utambuzi na utoaji huduma za posta nchini.

"Serikali imejielekeza katika kuhakikisha kwamba tunakuwa na miundombinu rafiki katika usafirishaji na ugavi mfano serikali imewekeza fedha nyingi katika kuunda mfumo wa 'postcode' na anuani za makazi. Ningependa kuwashirikisha kwamba nchi nzima sasa ina 'postcode'zake" alisema.

Alibainisha kuwa mfumo wa misimbo ya posta Tanzania (Postcode Tanzania) sasa utakuwa katika ukamilifu na kuwezesha utoaji huduma za posta na ufikishaji wa vifurushi na vipeto katika maeneo ya makazi, ofisi na sehemu za biashara.

"Pia utatumika katika utoaji wa huduma nyingine za jamii zikiwemo huduma za kutoa taarifa kwa zimamoto, polisi na kadhalika," alisema.

Msimbo wa posta, alisema ni namba iliyochaguliwa kwa kila kata nchini na kupitia mfumo huo, kila kata ina msimbo wa tarakimu tano lengo ni kuhakikisha kila barua au kipeto kinachotumwa nchini kionyeshe namba hiyo juu ya bahasha au kifurushi kwa ajili ya urahisi wa kufikisha mzigo au barua husika panapostahili.

Awali Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Dk. Jabiri Bakari, alisema TCRA imejizatiti kuhakikisha huduma za posta zinakuwa zenye ushindani kwa kuongeza ufanisi.

Alisema mamlaka hiyo tayari imetoa leseni za huduma za posta kwa watoa huduma 119, kote nchini ambao wanatoa huduma ya kusafirisha vipeto na mizigo isiyokuwa barua ndani ya nchi, Afrika Mashariki na kimataifa.

Mkuu wa Kitengo cha Posta katika Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Haruni Lemanya, akiwasilisha mada kwenye warsha hiyo, alisisitiza umuhimu wa watoa huduma za posta hasa wanaosafirisha vifurushi na vipeto kuhakikisha wanatumia mbinu za kisasa na zenye weledi wakati wote.



# Mwinyi aeleza kutoridhishwa utendaji kazi wa TAMISEMI

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameeleza kutoridhishwa na utendaji kazi wa Mamlaka za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa yakiwamo Mabaraza ya Miji na Manispaa za Zanzibar.

Aliyasema hayo juzi alipokutana na viongozi wa serikali za mitaa kutoka mikoa yote ya Zanzibar wakiwamo wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya zote za Unguja na Pemba, Ikulu Zanzibar.

Dk. Mwinyi alisema lengo la kikao hicho ni kuhakikisha mabadiliko chanya yanatokea hasa katika halmashauri za Unguja na Pemba sambamba na kuimarisha utendaji wa kazi kwa azma ya kuwahudumia wananchi ipasavyo.

Katika mazungumzo hayo, Rais Dk. Mwinyi alizitaka kila halmashauri ihakikishe inatekeleza ipasavyo majukumu yake ikiwa ni pamoja na kusimamia makusanyo ya mapato na kuwataka wakuu wa mikoa na wilaya kusimamia hilo ili fedha hizo zisaidie shughuli za maendeleo.

Aliyataja majukumu ya serikali za mitaa kuwa ni pamoja na kusimamia usafi katika maeneo yote ya miji ya Zanzibar ikizingatiwa kwamba Zanzibar ni eneo maarufu la utalii.

Rais Dk. Mwinyi alisema makusanyo ya halmashauri ni lazima yatumike kwa ajili ya maendeleo ya nchi na wananchi wake.

Alizitaka manispaa zote za Unguja na Pemba kuhakikisha miji inakuwa safi huku akiutaka uongozi wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuwahamasisha wananchi kufanya usafi katika maeneo yote wanayoishi yakiwamo ya biashara.

Aliagiza kuwa wafanyabiashara wadogo kupangwa vizuri na kusisitiza kufanya biashara katika maeneo maalum yaliyopangwa.

Rais Dk. Mwinyi pia alieleza azma yake ya kuendelea kuwasaidia na kuwaunga mkono wajasiriamali kwa kutoa Sh. bilioni 70 zilizotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) kwa ajili ya kuwasaidia huku akibainisha kuwa wenye jukumu la kusimamia fedha hizo ni serikali za mitaa.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Alhaj Dk. Hussein Ali Mwinyi, akifungua mlango wa Masjid Tawba Kisauni Wilaya ya Magharibi "B" Unguja, baada ya kuuzindua rasmi jana na kujumuika na waumini wa Dini ya Kiislam katika Sala ya Ijumaa. **PICHA: IKULU**

# Sweden kusaidia Zanzibar maendeleo elimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imetiliana saini na serikali ya Sweden msaada wa dola za kimarekani milioni 5.4 zitakazotumika kuimarisha elimu ya msingi na maandalizi na kujenga uwezo wa wanafunzi kupata elimu ya vitendo.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Juma Maliki Akili, alitia saini kwa upande wa Zanzibar huku Sweden iliwakilishwa na Balozi wake nchini, Anders Sjoberg. Utiaji saini wa msaada huo ulifanyika jana katika ofisi ya wizara, Vuga mjini Unguja.

Balozi Sjoberg alisema nchi yake imekuwa mstari wa mbele katika kusaidia maendeleo ya sekta ya elimu Zanzibar katika nyakati tofauti kupitia shirika lake la misaada la kimataifa (SIDA).

Alisema miongoni mwa vipaumbele vya nchi yake kwa upande wa Zanzibar ni uimarishaji wa sekta ya elimu katika ngazi ya maandalizi na msingi hadi sekondari ili kutoa mafanikio mazuri ikiwamo ufaulu wa wanafunzi.

Katika ngazi ya elimu ya msingi, alisema kuna matatizo kadhaa ambayo ni kikwazo katika mafanikio ya wanafunzi ikiwamo idadi kubwa ya wanafunzi na uhaba wa madarasa.

"Msaada huu ni sehemu ya utekelezaji wa mkataba wa ushirikiano wa miaka mitano kuanzia mwaka 2021 hadi 2026 baina ya Zanzibar na Sweden wenye lengo la kuimarisha sekta ya elimu katika ngazi ya msingi na maandalizi," alisema. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohamed Said, alisema msaada huo utazipatia ufumbuzi changamoto katika sekta ya elimu pamoja na kujenga uwezo wa walimu kuleta ufanisi.

Alisema mahitaji ya walimu kwa sasa ni kuongeza uwezo wa elimu huku wizara ikijikita zaidi katika kutafuta walimu wenye uwezo wa kusomesha masomo ya sayansi na hisabati.

"Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatoa shukrani za dhati kwa serikali ya Sweden kwa msaada mkubwa ambao umelenga moja kwa moja kuboresha sekta ya elimu na kuleta matokeo mazuri ya ufaulu wa wanafunzi," alisema.

Naye Dk. Malik alisema sekta ya elimu ni miongoni mwa vipaumbele vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika bajeti yake kwa mwaka wa fedha 2021/22 iliyowasilishwa katika baraza la wawakilishi.

Alisema serikali imeweka mkazo mkubwa katika kujenga majengo ya kisasa yenye hadhi pamoja na upatikanaji wa vifaa vya maabara katika kuelekea kutoa elimu ya sayansi na teknolojia ya mawasiliano ya umma.

# Utekelezaji Ilani ya CCM wamkuna Shein

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MLEZI wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mjini na Mkoa wa Magharibi Kichama, Dk. Ali Mohamed Shein, ameelezea kuridhishwa kwake na utekelezaji wa Ilani ya CCM katika Wilaya ya Amani.

Akizungumza jana katika mwendelezo wa ziara yake ya kujitambulisha na kukagua utekelezaji wa Ilani ya Chama katika Tawi la CCM Kwa Sebleni, Unguja, alisema viongozi na wanachama ndani ya wilaya ya Amani wamefanya kazi kubwa ya kuimarisha chama kwa kuanzisha miradi mbalimbali ya maendeleo.

Dk.Shein alisema katika maeneo mbalimbali aliyoyatembelea na kukagua ameona miradi ya maendeleo inayotatua kero za wananchi wa maeneo husika.

Alisema miradi inayotekelezwa ikiwamo ya upatikanaji wa maji safi na salama, vikundi vya ujasiriamali, ujenzi wa maskani za kisasa za CCM na uendelezaji wa madarasa ya itikadi, mafunzo na elimu ni miongoni mwa mikakati endelevu ya kuimarisha chama na wanachama kujitegemea kiuchumi.

Aliwapongeza wabunge, wawakilishi na madiwani wanaoshiriki kutekeleza miradi hiyo ambayo ni sehemu ya utekelezaji wa ahadi walizotoa kwa wananchi wakati wa kampeni za uchaguzi uliopita.

"Nimepewa jukumu na CCM niwe mlezi wenu na nimekuja hapa kujitambulisha. Nimeanza kwa ngazi za chini kabisa za matawi na mashina, waliko wanachama wetu ambao ndio chimbuko na uimara wa chama," alisema.

Alisema serikali ya Zanzibar kwa awamu mbalimbali imekuwa ikitekeleza miradi ya upatikanaji wa huduma za maji safi na salama ili kuhakikisha changamoto hiyo inapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

Dk. Shein aliwasihi wanachama kununua bidhaa zinazotengenezwa na vikundi vya wajasiriamali vinavyoanzishwa na wanachama ili mitaji yao ikue na wajitegemee.

Dk.Shein ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa CCM Zanzibar, alisema katika juhudi za kuimarisha Chama ni lazima wanachama walipe ada kwa wakati na kusisitiza wanachama kuendelea kupendana na kuheshimiana na kuweka bayana kwamba chama hakiwezi kujengwa kwa kuchukiana.



R. KELLY AZIDIWA NA UPWEKE Uk.14







ITAKUWAJE

# Ali Kiba, Esha Buheti wakikosana?

JUZI ilikuwa siku maalum kwa mwanamuziki wa Bongo Fleva, Ali Kiba, wakati alipozindua rasmi albam yake mpya 'The Only One King' kwa mbwembwe nyingi.

Hata hivyo, shamrashamra hizo ziligeuka kuwa mwiba kwa mwanamuziki huyo baada ya kuibuka mvutano mkali kati yake na rafiki yake wa karibu Esha Buheti, ambaye ameonekana kukasirishwa na utaratibu mzima wa sherehe hizo za uzinduzi.

Esha alilalamika kuwekwa nyuma na Ali Kiba, muda wote kiasi cha kushindwa kutambulishwa wala kuwa miongoni mwa watu anaowashukuru, hivyo aliamua kuweka wazi kwamba atajiondoa kuwa shabiki wake.

Mzozo huo ambao umeharibu utamu wa uzinduzi wa Albam yake baada ya watu kuacha kufuatilia Albamu hiyo na badala yake kubaki wakijiuliza inakuwaje marafiki hao wanagombana hadharani.

Mashabiki ambao ndio wateja wakubwa wa wanamuziki hao, tangu juzi wamejikuta wakishabikia mgogoro huo na kuacha kuzungumzia kazi ya mwanamuziki huyo.

Hata hivyo Ali Kiba kupitia mtandao wa kijamii, alimuomba radhi kwa kasoro ndogo zilizojitokeza, jambo ambalo lilionekana kupokelewa kwa unyonge na Buheti, ambaye alisisitiza ataendelea na msimamo wake wa kuwa pembeni.

Baadhi ya wachambuzi wa sanaa, wanasema mzozo huo umeharibu mtazamo mzima wa mashabiki katika kazi hiyo, jambo ambalo si zuri kibiashara.

"Wakati wa uzinduzi wa Albam, msanii anatakiwa kuwa makini ili mashabiki wake muda wote waendelee kujadili kazi yake, lakini katika hali ya hivi sasa kati ya Ali Kiba na Esha Buheti, imeondoa ladha," amesema Abdul Matimbwa.

Amesema muziki sawa na biashara yoyote ambayo inatakiwa kutangazwa vizuri na pale inapotokea jambo zito wakati inapoanza kutangazwa lazima kuna mambo yatarudi nyuma.

"Kama ni kiki basi watakuwa wamekosea kwani wangejidhibiti kwa kuzungumza kimya kimya ili watu waendelee kujadili kazi badala ya watu," ameongeza kusema.

BASI SAWA

## Rayvanny atoboa siri ya Sallam



OFISA Mtendaji wa lebo ya Next Level Music, Rayvanny, amesema bosi wake katika lebo ya WBC, Sallam Sk, huwa hataki mchezo katika kazi.

Rayvanny amesema kuwa Sallam ana tabia ya utata kiasi ambacho wakati mwingine anapata wakati mgumu, lakini anatambua anafanya hivyo kwa sababu anataka afanye vizuri katika kazi.

Amesema bado yupo sana ndani ya WCB na ataendelea na kazi yake mpya katika lebo aliyoanzisha ambayo itakuza vipaji vya wanamuziki.

## Zabron warudisha hisani kwa wazazi


KUNDI la muziki wa Injili nchini, Zabron Singers, wamerudi kivingine na wimbo 'Nawapenda' maalum kwa wazazi wote.

Mwalimu wa kundi hilo Japhet Zabron, ameliambia BT, wimbo huo huo ulioachiwa jana unalenga kuwakumbusha watu kuwa wazazi ni watu muhimu kwenye maisha hivyo kuna kila sababu ya kuwaheshimu, kuwatunza na kuwalea kama ambavyo Mungu ameagiza.

Zabron Singers ni kikundi kinachoundwa na wanandugu na baadhi ya marafiki wachache wanaopatikana Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga katika Kanisa la Waadventista Wasabato.

Mwalimu Japhet Zabron amesema "Tangu Watanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla watupokee na kutukubali tufany baraka kwenye maisha yao tumejitahidi kuhakikisha hatujawaangusha katika mwendelezo wa matoleo ya nyimbo mpya,"






## Zuchu, Nandy jino kwa jino

SASA ule ubishi wa nani zaidi kati ya wanamuziki nyota wawili wa kike nchini, Zuchu na Nandy, utapata jibu hivi karibuni.

Wasanii hao ambao wanaongoza kwa kupendwa na mashabiki, wametajwa kuwania tuzo za AFRIMMA kwenye kipengele kimoja.

Zuchu na nandy watakutana katika Kipengele kimoja cha "Msanii Bora Wa Kike Afrika Mashariki" ambapo mshindi ataibuka na tuzo.



## Amber Lulu kwa hili umezidi!

MWANAMUZIKI na mpambaji wa video, Amber Lulu, amesema hana muda wa kuzaa watoto wengi kwa mwanamume mmoja, kwani anaweza kufa kwa mawazo.

Amesema lengo lake ni kupata watoto watano kila mmoja na baba yake, ili iwe rahisi kuhudumiwa endapo baba mmoja akifariki dunia.

"Nikizaa na mwanamume mmoja nitapata tabu kuwalea endapo atafariki, nimepanga kuwa na watoto hao kila mmoja na baba yake nipate urahisi wa kuwatunza," amesema.

## Ngoma 5 Septemba usipime

**Na Adam Fungamwango**

MWEZI Oktoba umeingia, Septemba umeondoka kwa mbwembwe huku ikishuhudiwa ngoma kali zilizotolewa na wasanii mbalimbali nchini.

Ulikuwa ni mwezi wa kushindana, huyu akitoa hiki na yule anatoa kile. Si kwa wasanii wote, ni kwa wale waliojiandaa.

Tumeshuhudia ngoma kadhaa ambazo kwa sasa zimeanza kushika chati kwenye majedwali na chati za muziki kwenye televisheni na redio mbalimbali, hata mitandao ya kijamii.

Hizi ndiyo ngoma kali kutolewa mwezi Septemba, pamoja na wasanii waliofanya hivyo.

**NAANZAJE-DIAMOND PLATINUMZ**

Mwezi Septemba ulianza kwa kishindo kwa wasanii wa muziki wa kizazi kipya, bongo fleva. Ni pale mashabiki wa muziki huo waliposhuhudia msanii maarufu zaidi Afrika Mashariki na Kati, Dimond Platinumz alipotoa ngoma yake 'Naanzaje'. Kama ilivyo kwa wasanii au wanamuziki bora kabisa duniani, si mara kwa mara kutoa singo au albamu. Lakini anapokuja kutoa kunakuwa na mtikisiko kwa sababu kila mmoja, mashabiki, wafuasi na hata wapinzani wanataka kuangalia nini ametoa.

Wengine kwa ajili ya kupata burudani, wengine kwa ajili ya kusifia, na wapinzani wanaisikiliza kwa ajili ya kuponda tu. Ilikuwa ni Septemba 5, Diamond alipotoa ngoma hiyo, ambayo pia imeambatana na video kali iliyopamba 'pini' hiyo.

**SINA NENO-JUX**

Msanii Jux hakuwa nyuma kwenye mwezi Septemba. Ametoa ngoma yake tarehe 22, ambayo ameiita 'Sina Neno'. Ni wimbo wa mapenzi. Hata hivyo ameiimba kwenye mahadhi ya taratibu kiasi cha kwamba inafaa zaidi kuisikiliza, lakini siyo kuicheza.

**SIZE YAO-DARASA FT DOGO JANJA**

Ni mchanganyiko wa waimbaji wa nyimbo ngumu. Hao ni Darasa akimshirikisha Dogo Janja, ngoma inakwenda kwa jina la 'Size yao'.

Imeachiwa Septemba 24 na tayari imeshaanza kubamba sehemu mbalimbali za starehe na kwenye sherehe mbalimbali. Maudhui ya ngoma hii ni ya majigambo zaidi.

**WEKAWEKA-BELLE 9**

Amerudi upya kabisa. Ni Belle 9 yule wa zamani. Septemba 24 ametambulisha ngoma yake iitwayo 'Wekaweka'. Kama kawaida ya nyimbo nyingi za bongo fleva ni za mapenzi.

Mapigo ya ngoma hii ni ya kuchezeka, hivyo yanafaa kabisa kuweka kwenye kumbi au sherehe kwa ajili ya kuchizisha mashabiki.

**YUDA-NANDY**

Mrembo Nandy naye hajapoa kwenye mwezi Septemba. Mwishoni kabisa mwa mwezi, tarehe 30, akaibuka na ngoma yake. Inaitwa 'Yuda'. Ni ngoma ya mapenzi pia. Ukiisikiliza ngoma hii, uimbaji na mapigo yake utaona kuwa wasanii wa Tanzania wameanza kubadilika kutoka kwenye mapigo ya kimagharibi, au Kinaigeria na kwenda kwenye kutafuta utambulisho wao, na hasa wasanii wa kike.

Ndani kuna vinanda na vinubi. Ni aina na mapigo ya 'Kizuchuzuchu hivi'. Wasanii hawa wawili, wanaweza kupeleka muziki wa Kitanzania mbali sana.






## Mjumbe Kichefuchefu; Akilianzisha presha tupu

**Na Adam Fungamwango**

SERIKALI imeweka wajumbe wa nyumba kumi kwa ajili ya kutatua matatizo kwenye ngazi za chini. Jambo au tatizo lolote hutatuliwa kwa mujibu wa sheria, lakini mwanzo kabisa wajumbe hujitahidi kulitatua kwa busara au utamaduni wa eneo husika, ili mradi tu isivunje sheria za nchi.

Wengi wanafanya kama ilivyo. Lakini kuna wachache badala ya kufanya hivyo wanajitengenezea ufalme wao. Hujifanya ndiyo polisi, washtaki na mahakama, badala ya kusuluhisha au kulipeleka kwenye ngazi husika.

Filamu ya 'Mjumbe Kichefuchefu', inaangazia baadhi ya wajumbe wa nyumba kumi wasio na maadili. Imechezwa na wasanii Tin White, Ringo, Mau Fundi, Babu Majanga, Masantula na wengineo.

Tin White ni mjumbe wa nyumba kumi. Lakini kwenye eneo lake watu wanakoma. Amejitengenezea ufalme na sheria zake mwenyewe. Amejitungia kanuni zake mwenyewe ambazo ni kero na maumivu kwa watu wa eneo lake.

Kwanza kabisa kuna mtu na mpenzi wake waliwenda kwake. Badala ya kusuluhisha, akawaambia wote wana makosa, hivyo wanatakiwa kulipa faini. Mwanamume alilipa, lakini mwanamke hakuwa nayo. Akaambiwa aache simu na akipata ataleta. Akahalalisha uchezaji wa kamari kwenye eneo analoongoza kwa sharti ya kulipa ushuru.

Mjumbe alikutana na mwanamume yule, akamdanganya kuwa amepostika kwenye mitandao ya kijamii na kuchafuliwa jina lake, hivyo ana wasiwasi naye au yule demu wake kumposti.

Kwa kuwa jamaa hakufanya hivyo, akadhani kuwa huenda ni mpenzi wake waliyepelekana kwa mjumbe ndiye amefanya hivyo.

Mbaya zaidi akaruhusu kisirisiri wezi kufanya uhalifu, lakini wawe wanampelekea pesa tu nyumbani kwake.

Halafu mjumbe mwenyewe anatembea na bonge la bodigadi baunsa, utafikiri msanii wa bongo fleva.

Hii iliwafanya wakazi wa eneo lake kumchukia mjumbe wao, kwani hakuna anachokifanya, bali unapokwenda kushtaki, mshtaki na mshtakiwa wote wanaonekana wana makosa.

Hali ilizidi kuwa mbaya, hadi wakaenda kushtaki kwa Mwenyekiti wa Serikali za Mitaa. Akaanza kufanya uchunguzi.

Hata baunsa wake sasa alianza kuwaonea wananchi huruma, akamtoroka. Mke wa mjumbe naye baada ya kuona kila anakopita anyooshewa vidole, akamuonya mumewe, baada ya kuona harekebishiki, naye akamkimbia. Mjumbe akabaki mpweke. Siku ya siku akaja kukamatwa na polisi, kukiwa na kundi la wananchi nje likiimba kuwa hawamtaki.



# R. Kelly azidiwa na upweke

HALI ya upweke inazidi kumwandama mwanamuziki nyota wa Marekani, Robert Kelly, maarufu kama R.kelly, baada ya watu wake wa karibu kuanza kujitenga naye.

Hatua hiyo inakuja baada ya mahakama kumtia hatiani katika mashtaka ya unyanyasaji wa kingono na wasichana chini ya umri wa miaka 18.

Vyanzo vya karibu vinasema msanii huyo yupo kimya na amekuwa na mawazo mengi baada ya watu wake wa karibu kujitenga na kampuni kadhaa kufuta ushirikiano naye.

Hivi karibuni, mtandao wa kuweka maudhui, YouTube, umezifunga akaunti tatu za muziki za R. Kelly.



## Princess ukipata nyingine jilinde

MSANII wa filamu kutoka Ghana, Princess Shyngle, ametoa ufafanuzi kutokana na kupata tatizo la kuharibika kwa ujauzito wake.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Princess amesema tatizo hilo lilitokana na kudhoofika na kupasuka kwa mji wa mimba kutokana na kazi anazofannya.

"Baada ya kufurahia kwa wiki kadhaa na kujiandaa kwa ajili ya ujio wa mtoto wangu mwezi wa Desemba au januari, mambo yameharibika kutokana na matatizo ya kudhoofika kwa mji wa mimba," ameandika.

## Mary Njoku wewe kweli mzalendo

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Mary Njoku, amesema endapo atapewa maisha mengine, atachagua kubaki Nigeria kwa sababu anaipenda.

Kupitia akaunti yake ya Instagram, staa huyo wa filamu amesema hayo wakati akichangia majadala wa jinsi gani mtu analipenda taifa lake.

"Nigeria inaivunja roho yangu, katika maisha yangu yajayo bado nitasimama kuwa Mnigeria, tupo watulivu," ameandika.





## Davido kuiona kwenye TV AFRIMMA

MSANII mwenye mashabiki wengi barani Afrika, David Adedeji Adeleke, maarufu kama Davido, kwa mara ya kwanza amekuwa nje katika tuzo za AFRIMMA mwaka 2021.

Mara nyingi huwa tunamuona Davido katika vipengele ambavyo vinawakutanisha na mastaa wenzake kama Wizkid na Burna Boy lakini mwaka huu jina lake halipo katika tuzo hizo ambazo sherehe zake zitafanyika nchini Nigeria.

Majina yaliyotawala katika vipengele vyote ni Wizkid na Burna boy, ambao mmoja inawezekana akaibuka kuwa mwanamuziki bora kwa mwaka huu.

## 2Face atoa onyo kali

MSANII wa muziki wa Nigeria, 2Face Idibia, ametishia kufungua mashtaka dhidi ya Brymo, akilalamika kuchafua jina lake katika tweet zake.

Itakumbukwa kuwa Brymo katika mfululizo wa tweet zake, alimlalamikia msanii huyo wa muziki kwa kumshambulia baada ya kujua ana uhusiano wa kimapenzi na mke wake.

Brymo aliaindika kwenye ukurasa wake wa Twitter, siku ya Alhamisi, kuwa amepokea barua kutoka kwa 2face, akimuonya kuacha mara moja madai yake hayo.



MAKALA

# MPANGA KIPENGERE

# Pori la akiba linalotamba kwa vivutio utalii maua ya kipekee

**Na Christina Haule,**
ALIYEKUWA MAKETE

ENEO la Ibaga lililopo katika Pori la Akiba Mpanga-Kipengere, linalomilikiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), ni moja ya vivutio vya kipekee vilivyopo nchini kutokana na kuwa na maua ya aina tofauti.

Ni mimea inayoota yenyewe katika safu za milima, likiwamo au lijulikanalo kama Chikanda (orchids) linalopatikana Tanzania pekee duniani kote.

Mhifadhi Kiongozi kutoka kwenye pori la akiba Mpanga-Kipengere, Dominick Rwebangira, anasema eneo hilo lililopo ndani ya pori hilo la akiba lina vivuto vingi vya kitalii.

Licha ya kuwa na maua hayo yanayosadikiwa pia inayotumiwa kama chakula kwa nchi jirani ya Zambia na Malawi, inatumika kama dawa asilia ya kutibu magonjwa mbalimbali.

Rwebangira anasema, eneo hilo lina vivutio vingine ikiwamo wanyama wa aina tofauti, mbuzi mawe (kripspringer) na aina ya wanyama wadogo (stainbok) kama vile sungura pori, waliopo upande wa chini kwenye mawe.

Anasema kuna ndege mbalimbali wanaoruka kwa makundi na kutua kwa misimu mbalimbali kutoka mabara tofauti duniani, wakiwamo Tandawala Machaka (denharm bastard) na Blue Swallow.

Rwebangira anasema, eneo la Ibaga lililopo kwenye ukanda wa juu kwenye pori la akiba Mpanga-Kipengere, lina maua yamekuwa yakishamiri katika miezi ya Novemba hadi Machi, hivyo kufanya eneo hilo liendelee kuonekana bora wakati wote.

Anasema, uhifadhi wa eneo hilo la Ibaga kupitia pori la akiba la Mpanga- Kipengere umekuja baada ya kuwapo vyanzo vya maji vinavyotoka kwenye mto Kimani na mito mingine, inayopatikana kwenye milima Mpanga na Kipengere.

Licha ya utalii uliojitosheleza katika eneo hilo, bado linakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo ujangiri na uchomaji moto hovyo.

Anasema katika kukabiliana na hali hiyo wamekuwa wakifanya doria na kwamba eneo hilo linafikika kwa watalii baada ya kutembea umbali wa kilomita 15 kwa gari kutoka kwenye barabara kuu ya Dar es salaam-Mbeya.

Anasema katika kukabiliana na majangiri mwaka 2020 hawakukamata jangiri yeyote lakini mwaka 2021 wamekamata jumla ya majangiri wanne na kuwachukulia hatua mbalimbali za kisheria, ikiwamo kuwafikisha polisi na hatimaye mahakamani kupata adhabu ya kupewa faini na kifungo tofauti na zamani walikuwa wakipewa adhabu ya faini na baadae kurudia tena.



Mazingira ndani ya Pori la Akiba Mpanga-Kipengere. **PICHA: MTANDAO.**

Akizungumzia faida zingine za eneo hilo, Mhifadhi huyo anasema vyanzo vya maji vilivyopo kwenye mto Kimani huchangia kwa kiasi kikubwa, upatikanaji wa maji katika mabwawa makubwa na muhimu katika kuzalisha umeme nchini.

Anayataja mabwawa hayo ni Mtera na Kidatu na hivyo anawashauri wananchi wanaotumia maji hayo kwa namna moja au nyingine kuyatunza kwa manufaa ya Taifa.

Mhifadhi anasema, pia wamekuwa wakipokea wageni wanaofika kutalii katika eneo hilo na kuingiza fedha zinazosaidia kuinua maendeleo katika maeneo mbalimbali nchini.

Anasema, licha ya kupata watalii zaidi ya 200 kwa mwaka ambao kati yao 150 hadi 160 ni wa ndani bado idadi ya watalii imeonekana kuwa ndogo licha ya vivutio vingi vilivyopo.

"Watalii wa ndani wakubwa walipa kiasi cha Sh. 4,000 kwa mtu mzima, mtoto anaingia bure na watalii kutoka nje ya nchi wanalipa kuanzia dola 15 ambazo ni sawa na Sh. 30,000" anafanua.

Hivyo, anaitaka jamii inayozunguka hifadhi hiyo kuacha mara moja kujihusisha na uharibifu katika eneo hilo kwa sababu wanaleta uharibifu na kusababisha mimea kutoweka na kuharibu vyanzo vya maji yanayotoka katika mito miwili mikubwa ya Kimani na Ipela, anayosema kuna vyanzo vingine vya maji ambavyo bado havijaendelezwa; Mlomboji, Machimbo na Mbarali.

Anasema eneo la Ibaga, linapakana na vijiji vya Imalilo, Kilanzi na Molonga ambavyo ndipo majangiri wamekuwa wakitoka na kuingia hifadhini kwa kushirikiana na nchi jirani.

**MHIFADHI WA PORI**

Mhifadhi Mwandamizi kutoka TAWA Mpanga-Kipengere, Alfred Kipondamali, anasema pori hilo lilipopo eneo la Maketea, Nyanda za Juu Kusini lina uoto wa asili pamoja na maua tofauti yakiwamo chikanda (orchids) pamoja na mazao aina mbalimbali yanayopatikana katika maeneo ya Ibaga na Imalilo.

Aidha Kipondamali anataja malengo ya kuanzishwa kwa pori hilo la Akiba Mpanga- Kipengere ni kutunza hifadhi ya vyanzo vya maji, pori hilo likichangia zaidi ya asilimia 40 ya maji yanayoenda kwenye mabwawa makubwa ya umeme ya Kidatu na Mtera, sambamba na Mwalimu Nyerere.


"Kkwa kifupi, maji haya yana matumizi tofauti. Baada ya kutoka hifadhini, huwa yanaenda kwa ajili ya shughuli za kilimo katika Wilaya ya Mbarali, yanaingia Mto Ruaha, yanaenda katika Bwawa la Mtera, ambako yanazalisha umeme na yanaenda Bwawa la Kidatu na kwenda kwenye Bwawa la Mwalimu Nyerere," anasema.

Kipondamali anasema, pori hilo lilianzishwa mwaka 2002 likiwa na ukubwa wa kilomita za mraba 1,524 ndani ya mikoa ya Mbeya kwenye Wilaya ya Mbarali na kwenye wilaya za Wanging'ombe na Makete mkoani Njombe.

Kaimu Kamishna msaidizi mwandamizi wa uhusiano kwa umma wa TAWA, Twaha Twaibu, anawahimiza wazazi umuhimu wa kutalii, kwa kuwapeleka watoto kwenye vivutio vya utalii nchini wajifunze.

"Tuwapeleke watoto wetu kwenye kuangalia vivutio vya utalii vilivyopo, isijefika mahali mtoto anakuwa mkubwa akiulizwa yule mnyama gani, anatamka mnyama mwingine, ni aibu," anasema Twaibu.

TAWA ina mapori ya akiba zaidi ya 20 inayoyatumia kutangaza vivutio vya kitalii nchini likiwamo pori la Mpanga Kipengere lenye wanyama, misitu, maporomoko saba ya maji, harufu nzuri, na mapango ya kihistoria.



Mhifadhi Kiongozi Dominick Rwebangira, akizungumza na wanahabari (hawapo pichani) wakati walipotembelea eneo hilo. **PICHA: CHRISTINA HAULE**

# MAONYESHO DUBAI EXPO2020

Na Joseph Mwendapole

## ● Fursa Tanzania kujitangaza duniani
## ● Utalii, SGR,mazao, madini kupaishwa



Jengo linalotumika kwa maonyesho ya DUBAI EXPO 2020. **PICHA : MTANDAO**

MAONYESHO ya kimataifa ya biashara maarufu kama DUBAI 2020 EXPO, tayari yameng'oa nanga huko Dubai ambapo mataifa 191, ikiwamo Tanzania yamethibitisha kushiriki kuonesha bidhaa na fursa zinazopatikana kwenye mataifa hayo.

Kwa kawaida maonyesho hayo huanza Oktoba na kwenda hadi Machi mwaka unaofuata ili kuzipa nafasi nchi shiriki kuonyesha kwa kina fursa zinazopatikana nchini mwake na bidhaa zake.

Hata kabla ya maonyesho haya yaliyoanza Oktoba Mosi, Dubai ni sehemu ambayo dunia nzima inakutanishwa kutokana na namna ilivyosheheni mkusanyiko wa watu wa mataifa mbalimbali idadi kubwa ikiwa ni wafanyabiashara.

Dubai ni sehemu ndogo ndani ya Falme za Kiarabu (UAE) iliyoko katikati mwa mashariki ya kati yenye idadi ya watu wasiozidi milioni 3.5, lakini ilivyosheheni vivutio kem kem vya utalii, yenye ustaarabu wa hali ya juu kutokana na kutokuwa na matukio ya mara kwa mara ya uhalifu.

Kwa wasioifahamu vyema Dubai ni sehemu ya muungano wa mataifa saba yanayounda (UAE), ambayo ni Dubai, Abudhabi, Shalja, Agman, UmAlqudium, Fujiarah na Ras Al Khaima ambayo yanazungumza kiarabu.

Kwa Tanzania kushiriki maonyesho ya DUBAI EXPO 2020, ni fursa kubwa ya kuitangaza nchi ulimwenguni na nafasi za kiuwekezaji zilizopo nchini na miradi mikubwa ya ujenzi wa mindombinu kama ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) na bwawa la kuzalisha megawati 2,150 la Mwalimu Nyerere (JNHPP), Rufiji Pwani.

Maonyesho hayo makubwa ya kidunia ambayo hufanyika kwa miezi mitatu hadi sita na huratibiwa na Shirikisho la Maonesho Duniani Bureau of International Expositions (BIE).

Hii ni fursa nyingine kwa Tanzania kutumia Jukwaa la EXPO2020 kutangaza na kutafuta fursa za uwekezaji, masoko ya bidhaa zinazopatikana nchini, utalii na maliasili, utamaduni na mila na desturi na kujifunza mambo mbalimbali ya kibiashara na teknolojia.

Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Ukuzaji Biashara wa TanTrade, Getrude Ngwesheni, aliwaambia wahariri na waandishi wa habari hivi karibuni kuwa kwa kushiriki maonyesho hayo Tanzania itatangaza lugha ya Kiswahili na utamaduni kwa washiriki wapatao 207,600 na kutangaza miradi mitatu ya kipaumbele inayovutia uwekezaji.

Anasema hatua ya serikali kushiriki maonyesho hayo itasaidia kuimarisha biashara na masoko ya bidhaa na UAE kwa bidhaa za matunda kama parachichi, mikunde, maharagwe, mbaazi na kunde, chai, kahawa, nyama ya mbuzi, korosho, nguo, samaki, maua na karafuu.

Anasema Tanzania inafursa ya kuongeza mauzo ya bidhaa katika soko la UAE na Jukwaa la EXPO2020 Dubai linatoa fursa kwa Tanzania kupata mikataba na kuongeza mauzo ya bidhaa za matunda.

Aidha, anasema kwenye banda la Tanzania, washiriki watakaotembelea wataona makumbusho ya kihistoria, msikiti wa Kilwa, viongozi waliopita, mnara wa askari na vivutio mbalimbali vya utalii wa Tanzania.

Anaeleza kuwa banda la Tanzania litajumuisha washiriki kutoka taasisi za umma na binafsi watakaoonyesha mazao, bidhaa na miradi ya serikali na kampuni za uzalishaji wa bidhaa nane na sanaa zilizothibitisha ushiriki na bidhaa 137 zilifanikiwa kuingizwa katika mfumo wa mauzo wa EXPO2020 Dubai na bidhaa hizo zitajumuisha ngozi, chai, kahawa, mkonge, korosho, viungo na bidhaa za mikono ikiwamo milango ya Zanzibar.

Anasema siku maalum ya Tanzania imepengwa kufanyika Februari 26 mwakani na kutafanyika kongamano la biasharana uwekezaji kwa ushirikiano wa wizara za kisekta na taasisi za sekta binafsi ili kufanikisha maonesho hayo.

Ni fursa gani zinazoweza kupatikana Dubai

Dubai ni mji mdogo lakini wenye maajabu lukuki kwani wameweza kutengeneza bahari bandia katikati mwa mji, walifanikiwa kuchimba kiasi cha kilomita nne na kuunganisha eneo hilo na maji ya bahari kisha kutengeneza eneo maarufu kwa watalii kama Marine Parks.

Hili ni eneo maarufu na la kushangaza sana kwani inamchukua mtu muda kuamini kwamba bahari hiyo katikati ya Jiji si ya asili bali ni ya kutengeneza kutokana na umahiri mkubwa uliofanywa na wabunifu wa aneo hilo linalosheheni watalii.

Miongoni mwa maeneo mengine ya kuvutia nchini Dubai ni bustani ya maajabu maarufu kama Miracle Garden, kama inavyojieleza kwa jina lake kweli ni bustani ya maajabu kutokana na ustadi na ubunifu mkubwa uliotumiwa na wataalamu kuitengeneza.

Eneo hilo nalo limekuwa kivutio kikubwa cha watalii hasa msimu wa baridi kwenda kushuhudia usanifu wa kipekee na wa kustaajabisha uliofanywa na wajenzi wa bustani hii ya ajabu duniani.

Eneo lingine lenye mvuto wa ajabu ni jangwa lililoko umbali wa kilomita 40 kutoka mjini Dubai ambapo watalii mbalimbali hutembelea huko msimu wa utalii kujionea wanyama mbalimbali kama ngamia kwenye eneo hilo maarufu kama Dubai Sunset Desert Safari.

Hili eneo limekuwa na mvuto wa kipekee hasa kwa namna magari yanavyosafiri ndani ya jangwa hilo kutokana na kuwa na miinuko mikubwa na mitermko mikali kiasi kwamba mtalii anaweza kudhani kwamba gari linaanguka.

Kutokana na eneo hilo kuwa na miinuko mikubwa na mitermko mikali kwa kawaida watalii hupelekwa na magari ya kisasa yanayosukuma magurudumu manne yaani four wheel drive kwani wenyeji wanasema magari mengine hayawezi kufika maeneo husika.

Maajabu mengine ya Dubai ni kitu kinachoitwa La Perle huu ni ukumbi wa maonyesho wenye maajabu ya kushangaza duniani ukiwa na jumla ya viti 1,300 uliojengwa chini ya hoteli. Ukumbi umetengenezwa kwa nakshi za ajabu kiasi cha kushangaza wengi wanaofika kushuhudia maonyesho ya sanaa yanayofanywa kwenye ukumbi huu.

Bwawa la kuogelea lililoko kwenye ukumbi huu ni majabu mengine kwani wasanii wamekuwa wakizama na wasionekane walikotokea. Katika onyesho la juzi watu zaidi ya 1,000 waliokuwa kwenye ukumbi huo walishikwa na butwaaa kuona mmoja wa vijana waliokuja kama watazamaji kutoswa kwenye bwawa hilo na kutoonekana tena.

Mbali na kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini kupitia DUBAI EXPO 2020, Serikali ya Tanzania inapaswa kufanya utaratibu huo kuwa endelevu kwa kuhakikisha inatumia njia na mbinu mbalimbali ikiwemo kutumia watu mashuhuri.

Tanzania imejaaliwa kuwa na rasilimali madini ya Tanzanite ambayo inapatikana hapa nchini tu lakini baadhi ya mataifa yamekuwa yakitumia udhaifu wa kutojitangaza vyema kuilaghai dunia kuwa madini hayo yanatoka kwenye nchi zao.

Hivyo fursa ya DUBAI EXPO 2020 ni muhimu kwa Tanzania kuiambia dunia kuhusu madini hayo na kuwaumbua mataifa ambayo yamekuwa yakihadaa dunia kuhusu madini hayo.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/MASHAMBA

**KIWANJA KINAUZWA,** KIPO KISUKURU JKT SEGEREA DAR ES SALAAM, UKUBWA **SQM 2252,** KINA HATI, BEI 60 MILIONI. **MAWASILIANO: 0655 857523.**

## NYUMBA/MASHAMBA

**KIWANJA KINAUZWA** ENEO TEGETA NAMANGA KARIBU NA BARABARA YA AL HASSAN MWINYI.MAWASILIANO NAMBA **0753029141 AU 0713440436**

**Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku**

## KUPOTEA KWA VYETI



**SAADA MUSSA** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo,cha kidato cha nne cha kurisiti chenye index namba **P0314-0086** kilichotolewa na **TABORA TEACHER'S COLLEGE CENTRE** mwaka 1996 na cheti cha kidato cha nne cha kurisiti chenye index namba **P0314-0043** kilichotolewa na **TABORA TEACHER'S COLLEGE CENTRE** mwaka 1997 na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0346-0599** kilichotolewa na shule ya secondary **UYUI HIGH** mwaka 1998, yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **MWA/MAG/RB/428855/2021**

116501702

**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**DAR ES SALAAM**

**UTHIBITISHO WA USIMAMIZI WA MIRATHI**

**MIRATHI Na 119 YA MWAKA 2021**

**MAOMBI YA BARUA ZA USIMAMIZI WA MIRATHI YA MAREHEMU**

**MOHAMED ABDALLAH WILLI DAYA**

**MWOMBAJI/WAOMBAJI**

**SULATANA MOHAMED ABADALLAH WILLI DAYA**

**TAARIFA YA KAWAIDA**
**(Kanuni ya 75)**

Watu wote wanaodai kuwa na haki ya Marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia mashauri haya katika Jalada kama wanaona inafaa kabla ya kutolewa kwa uthibitisho wa barua za usimamizi wa Mirathi kwa Waombaji/Mwombaji hapo juu.

Mapingamizi yoyote kuhusu haya yawe yameandikishwa Mnamo au kabla ya tarehe 8 Mwezi wa 11 2021
Imewasilishwa Dar es Salaam, leo tarehe 8 Mwezi wa 10 2021

**NAIBU MSAJILI**

**NAKALA KWA**
**SULATANA MOHAMED**
**ABDALLA WALLI**
**DAYA**

NAIBU MSAJILI

116503502

## TANGAZO LA NOTISI - WADAIWA SUGU

**TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICE LIMITED,** Inatangaza notisi ya siku Sitini (60) Kuanzia tarehe ya Tangazo hili. Hatua zaidi za Kisheria zitachukuliwa kwa wadaiwa watakaoshindwa kulipa madeni yao ndani ya muda ulioainishwa( siku sitini).Ikiwa ni pamoja na kuwaruhusu madalali kuuza mali zao ambazo zimetumika kama dhamana za mikopo.

**Wadiwa ni:**

1. Elizabeth Edward Matemba - Kimara (DSM)
2. Jerome Jerome Tesha – Utunge mwago (Mkuranga)
3. Pascal Linus Kimolo – Kitunda (DSM)
4. Rashid Kessy Mangirile- Kigamboni (DSM)
5. Omari Said Magoma/Mwajuma Charles Magori- Mbagala (DSM)

**Mawasiliano piga:**
**222774742-3/0718068335**
**Au Email: tujijengetanzania@tujijenge.or.tz**

116503002

## TANGAZO LA NOTISI KULIPA DENI

**TUJIJENGE TANZANIA FINANCIAL SERVICE LIMITED,** Inatangaza notisi ya siku Thelathini (30) Kuanzia tarehe ya Tangazo hili. Hatua zaidi za Kisheria zitachukuliwa kwa wadaiwa watakaoshindwa kulipa madeni yao ndani ya muda ulioainishwa( siku thelathini).Ikiwa ni pamoja na kuwaruhusu madalali kuuza mali zao ambazo zimetumika kama dhamana za mikopo.

**Wadaiwa ni:**

1. Trazian Ishengoma Bernard (Chesco D.Mpiluka)
2. Agnes Ali Njama (Jerome Jerome Tesha)
3. Abdul Mohamed Karishi
4. Lisa Lazaro Nyato
5. Arafa Hussein Abdallah

**Mawasiliano piga:**
**+255 222774742-3/0718068335**
**au Email: tujijengetanzania@tujijenge.or.tz**

116503002

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**HAMISI ATHUMANI MBALALE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SUZUKI GRAND VITARA** yenye namba za usajili **T 727 CBP**, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **ARU/ARU/RB/486471/2021**

116503402

## KUPOTEA KWA CHETI



**RASHIDI IBRAHIMU** anatangaza kupotelea na cheti cha UALIMU chenye index namba **E.534/059** kilichotolewa na chuo cha UALIMU MTWARA mwaka 1982,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi taarifa **MTW/MTW/RB/479029/2021**

116487802

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **BABE MICROFINANCE ltd, Champion Auction Mart Ltd** tutauza kwa mnada wa hadhara Mali za wadaiwa Sugu - BUNDA kama ilivyotangazwa kwenye gazeti, Lengo ni kufidia/ kupunguza madeni ya mikopo wanayodaiwa:-

| Mdaiwa/ Mthamini | Dhamana | Mahali Ilipo | Tarehe ya mnada |
|---|---|---|---|
| Simion Ong'oro | Kiwanja | Nyamakokoto | 27/10/2021 |
| Golani Manyama Juma | Nyumba | Bunda stoo | 27/10/2021 |
| Daudi Nyamhanga | Nyumba | Guta | 29/10/2021 |
| Choma Mkami **(Mdhamini)** / Mussa Isonzo | Nyumba | Balili | 29/10/2021 |
| Emeliana Jackson Mgogo | Nyumba | Lamadi-Busega | 30/10/2021 |

**Masharti ya mnada**

Minada itafanyika mahali dhamana zilipo kuanzia saa nne asubuhi. Mteja atalipa 25% siku ya mnada, 75% atalipa ndani ya siku 14 akishindwa kulipa 25% hairudishwi. Gharama za kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.

**Mawasiliano piga:-**
**Champion Auction Mart ltd – 0764310997**

116502702

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Khaled Athumani Rukola** mkazi wa Kambarage Manispaa ya Shinyanga.
Anatangaza kupotelewa na Kadi ya Gari yenye namba za usajili **T. 663 BQT Toyota HIACE,** Injini namba **Z212BF.**
Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu, au awasiliane na Khaled Atumani Rukola kwa simu namba **0767674361.**
**Rbnamba/Shy/RB/2021/ Control namba 9910830529354.**

116502402

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**FRANK PASCAL MENDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HIACE COMMUTER** yenye namba za usajili **T 417 DBG.** Chassis No. **RZH1241000425, Engine No.1RZ0688545.** yeyote atakayeiona atoe taarifa cha Polisi. Taarifa ya Polisi **DOD/DOD/RB/485497/2021.**

116486602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MOROGORO**
**LILILOPO MOROGORO**

**MAOMBI MAGODO NAMBA 488 YA 2021**

**TRETEM NETWORK OF SCHOOLS .............MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**SAMWEL EDSON KAHAMBA**
**AMINA SHIZA KAYANDA**
**JUMANNE JUMA..................WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**

**AMINA SHIZA KAYANDA**

**JUMANNE JUMA** Popote Mlipo mnaarifiwa mfike katika Baraza la Ardhi na Nyumba la Wilaya ya Morogoro tarehe 01/11/2021 mbele ya mwenyekiti E.Mogasa nyinyi wenyewe binafsi au mtume muwakilishi wenu bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa. Endapo hamtahudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uamuzi.
Imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza leo tarehe 08 mwezi October 2021

E. MOGASA
MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO.

116502102

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**JULIUS RAPHAEL DETEBA**
Anatangaza kwa kupotelewa kwa kadi zake za magari zenye namba za usajili ni;
**T 918 AHQ, T 432 AKS, T 658 AGE, T 608 AGQ**
Kwa yeyote atakae ziona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Rb Namba.
**MOR/MOR/RB/485270/2021**

116502002

**MAHAKAMA YA MWANZO**
**MBARAMWO**
**S.L.P. 74, MUHEZA**
**6/10/2021**

**Kumb. NS. MBPC /NDOA/TALAKA/33/2021**

**YAH: SHAURI LA NDOA/TALAKA NO. 33/2021**

**MDAI – JULIUS SENGOE MFUKO**

**DHIDI YA**

**MDAIWA SOPHIA IRENE SHEMAKAME**

Tafadali husika na somo tajwa hapo juu. Mdai alifungua shauri hilo tarehe 22/9/2021 na kwakua mdaiwa hapatikani, kupitia gazeti lako unaombwa kumfahamisha mdaiwa kufika katika mahakama ya mwanzo mbaramo (Muheza) tarehe 22/10/2021 saa 2:30 asubuhi siku ambayo kesi itatajwa kwa mara ya kwanza.

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MBARAMO

116503502

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**ABDALLAH MOHAMED SALEH**
Anatangaza kwa kupotelewa kwa kadi yake ya Gari aina yake **TOYOTA-KLUGER** yenye namba za usajili **T 556 DWS**
**MODEL NO:ACUZ**
**CHASSIS NO:ACU200014137**
**ENGINE NO:2AZFE25478**
**BODY TYPE: STATON WAGON**
Kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Rb
**Namba.MOR/MOR/RB/483517/2021**

11650152

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**MACLEAN K MBONILE** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SUZUKI ESCUDO** yenyenamba za usajili **T 901 AKC** chasis namba **TDOIW281685** engine namba **GI6A431477,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi, Polisi taarifa **KW/RB/4770/2021**

116501802

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**BRAND DISTRIBUTORS LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya PULSAR yenye namba za usajili **MC 411 AEF** engine namba **DJGBTCO9637,** chasis namba **MDZDHDJ22TCC71088,** yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi,Polisi taarifa **DSM/PHQ/RB/485946/2021**

116502902

**OFISI ZA MATANGAZO**
**Mikocheni Industial Area,**
**Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.
Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake imekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.
Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka Mke Wangu-14

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Alishusha pumzi kwa nguvu. Tedi alimtazama kwa huruma "Pole sana. Pole mpenzi." Alimtuliza.

Hakujibu kwa mdomo. Akatikisa kichwa. Kilichofuata ni video za picha ambazo Sam alitishia kuzisambaza. Na zilionekana kweli kumtisha Farida, akamkimbia mumewe kabla ya hata piko aliyopaka haijakauka mwilini.

Nadhani aliona angekuwa mgeni wa nani kama zingevujishwa. Tena wakati huo yeye akiwa mke wa mtu. Na inawezekana ikaonekana kuwa zilikuwa zimepigwa baada ya harusi, au siku chache kabla ya harusi.

"Mimi nadhani mpaka hapa Tedi sina deni na wewe. Nashukuru sana sana tu. Umenisaidia sana. Sina uhakika kama ningekuwa peke yangu ningefanikisha kabisa. Au nisingefanikisha kwa muda mfupi kama huu. Kilichonitoa Dar na kuja Moro ni kumsaka mke wangu. Nilimuona kwa njia ile ya kujibadilisha sura. Na nilitaka kujua ni kwa nini alinitoroka wiki moja baada ya harusi. Leo nimejua. Sina wa kumlaumu."

Maneno aliyoongea Tom kwa sauti ya huzuni, alianza kumliza Tedi. Aliangua kilio kana kwamba anaambiwa au anatuhumiwa yeye.

Ilibidi sasa Tom, aache simanzi aliyonayo na kuanza kumbembeleza. "Usilie Tedi. Haya yote ni ya dunia. Dunia ni tambala bovu. Lakini ipo siku yataisha na itabaki simulizi na kuandikwa tu kwenye vitabu na magazeti."

Walijikuta wakikumbatiana. Wakaachana na simu, makaratasi pamoja na picha. Waakaanza kubembelezana. Kila mmoja akimbembeleza mwenzake. Usingizi mororo ukawapitia.

*************************

"Mpenzi nina wazo?" Tedi alisema akiwa amekaa kitandani akitafuna chapati kavu.

Wakati huo Tom alikuwa bado hajaamka kitandani, ingawa alikuwa macho.

"Wazo lipi?"

"Tungemsikiliza kwanza mkeo anasemaje."

"Atasemaje? Mimi sitaki hata kumsikiliza."

"Hapana mpenzi Tom usiwe na hasira. Kwa hili lililotokea ukiliangalia sana mkeo hakuwa na kosa.

Yeye alitaka ndoa, Sam hakutaka kumuoa. Au alichelewa. Akaondoka Moro akaja Dar. Akakutana na wewe. Ukakolea, ukatangaza ndoa. Kumbe wakati huo ana mgogoro na bwana yake ambaye alikuwa naye kabla yako. Alikataza lakini akalazimisha kuolewa kwa nguvu. Kumbe wakati wa mapenzi yao walikuwa wakijipiga picha ambazo si nzuri. Bwana katishia kuwa asipoondoka kwako atavujisha picha chafu. Na kweli jinsi tulivyoziona zingemchafua hasa. Na hata wewe ungeziona kwenye mitandao ya kijamii, sidhani kama ungeendelea kuwa naye. Ni aibu aisee. Hata kama ungeamua wewe kuendelea naye, lakini wazazi au ndugu na jamaa zako wasingekuwa radhi naye," Alikuwa akiongea kwa utulivu huku akiendelea kuiteketeza chapati yake isiyokuwa na supu, wala chai.




**"Tom, mimi si nimechukua simu ya Sam. Unadhani hakuna namba yake? Kwenye meseji hizi ambazo tulikuwa tunasoma, namba walizokuwa wanatumiana si zinaonyesha?"**

Tom hakujibu chochote. Alibaki anamtazama tu Tedi. Mwanamke ambaye kwake binafsi aliona ni kama aliletwa zawadi kwa ajili ya kumsaidia tatizo lake la kusaka mkewe Farida. Hakuamini kama ushahidi wote wa picha za mnato, video na nyaraka kadhaa kwenye karatasi, ikiwemo simu ya mkononi angeupata kirahisi kama angekuwa peke yake bila yeye. Labda kwa kumteka nyara Sam.

'Mimi navyoona aliamua kukutoroka kwa ajili ya picha zake zisisambazwe kwenye mitandao ya kijamii na kulinda ndoa yake isivunjike. Ndiyo maana nakushauri kwanza tumsikilize kwanza anasemaje. Unajua nikwambie mpenzi, haya mambo yanatokea kwenye maisha. Si wanawake wengi wanakwenda kuolewa wakiwa hawana wapenzi huko nyuma. Unakuwa na wapenzi kadhaa, lakini unamchagua mmoja, ndiyo anakuwa wako wa maisha. Hata wanaume pia. Kwake imekuwa ngumu kwa sababu jamaa ni king'ang'anizi."

"Sasa kwa hili wewe unataka kuniambiaje, maana sikuelewi ujue." Kwa mara ya kwanza Tom aliongea.

"Tuongeaa naye tumsikilize, anasemaje, au anajitetea vipi kwa hili."

"Sina hata namba yake, maana alipotoroka aliacha kabisa kutumia namba hiyo na kila ikipigwa haipatikani. Nadhani aliamua kubadilisha hata namba."

"Tom, mimi si nimechukua simu ya Sam. Unadhani hakuna namba yake? Kwenye meseji hizi ambazo tulikuwa tunasoma, namba walizokuwa wanatumiana si zinaonyesha?"

"Wewe ulitaka tuongee naye nini kwa mfano?"

"Sikiliza, mimi nitachukua namba. Nitampigia, halafu nitaongea naye."

Tom kwa upande wake hakuona umuhimu wowote. Alikuwa ameshatumbukiwa nyongo. Kila kitu kwake kilikuwa kimeharibika. Ilikuwa ni rahisi tu kwake kumwambia Tedi kuwa aache. Asifanye kitu chochote. Lakini hakufanya hivyo. Kwake Tedi kwa wakati huo alionekana ni muhimu kwake. Ndiye angalau anamfanya kupumua na kuwa na stamina kwa kile ambacho kimetokea. Vinginevyo, ama anakwenda kuua mtu au watu. Au angejidhuru mwenyewe. Maumivu aliyoyapata, yalikuwa hayamithiliki. Tedi kwake ilikuwa ni kama barafu iliyopoza maumivu makali yaliyomkabili. Akajikuta akimjibu "Sawa, fanya unavyotaka. Kwa hili wewe utaniongoza nini cha kufanya."

Tedi alipiga simu kwa kutumia namba ambayo ilionekana ni ya Farida. Iliita.

"Nani mwenzangu." Alisikia sauti. Ilibidi Tedi abonyeze kitufe kinachookuza sauti ili Tom naye asikie.

"Naitwa Fetty."

"Wa wapi?"

"Msamvu hapa."

"Unasemaje?"

"Unamfahamu Tom?"

"Tom yupi?"

"Mumeo?"

Farida alisita kidogo na kujibu.

"Eeeh ndiyo."

"Kanituma nije nikuletee ujumbe wake kwa sababu namba ambaye ulikuwa unatumia haipatikani tena."

"Kwani wewe ni nani na namba hii umeipata wapi?"

"Mimi ni rafiki yako, tulikuwa wote tunaishi kule Kigamboni, ila huwezi kunijua. Nilikutana naye, ananiambia kama utakwenda Moro ukikutana na Farida mpe ujumbe wangu."

"Ni wa maneno au?"

"Hapana ni mambo fulani ameniambia nikwambie, lakini sitayasema kwenye simu, lakini ni muhimu sana."

"Ina maana amejua kama niko Moro?"

"Hapana, yeye mpaka sasa hajui yuko wapi. Ila stori za Dar huko ni kwamba ulimtoroka wiki moja tu baada ya harusi."

"Wnasemaje, wanajua sababu?"

"Hapana. Tutajuaje. Labda shoga tukikutana utaniambia."

"Tukutane wapi?"

"Sijui wewe?"

"Unajua mimi siku hizi natembea kwa tahadhari sana, kwa hiyo naomba tu kama unaweza njoo nyumbani kwetu hapa Msangani."

"Haina neno shoga nitakuja kukupatia ujumbe wako."

"Haya, mchana mwema."

"Nawe pia."

Alitaka simu. Akamtazama Tom.

"Tom, najua hupendi ninavyotaka kufanya, lakini naomba tufanye hivi kwa sababu tunaweza kupata kitu kingine ambacho hatukukitarajia."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# PRISONS YAJIPANGA UPYA LIGI KUU BARA

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Tanzania Prisons, Shaban Kazumba (pichani) amesema kazi kubwa wanayoifanya kwa kipindi hiki cha mapumziko ya kalenda ya Fifa ni kurekebisha makosa yao, ikiwamo umakini wa safu ya ushambuliaji kabla ya kurejea kwa Ligi Kuu.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kazumba alisema katika michezo miwili waliocheza, hawakupata matokeo mazuri na kuambulia pointi moja, huku walitengeza nafasi nyingi na kushindwa kuzitumia.

**Alisema wana matarajio makubwa ya mapumziko ya Fifa kufanyia kazi mapungufu yao na kuhakikisha timu yao, inarejea katika ubora zaidi ya msimu uliopita.**

"Hatukuanza ligi vizuri, tumefungwa mechi ya kwanza na kutoka sare, dhidi ya Mtibwa Sugar, michezo yote hiyo tumetengeneza nafasi nyingi, lakini tulishindwa kuzitumia, " alisema Kazumba.

Alisema ana imani mapumziko hayo, watayatendea haki kuhakikisha wanakuwa makini katika kutengeneza na kuimarisha kikosi chao, hasa kwenye safu ya ushambuliaji kwa kutumia vema nafasi wanazotengeneza.

Prisons ilianza vibaya kwa kufungwa bao 1-0, ugenini na Mbeya City katika uwanja wa Sokoine, na mchezo wa pili ilitoka suluhu na Mtibwa Sugar.






Mwanamuziki wa Muziki wa Dansi, Fallii Ipupa (kulia), akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, kuhusu onyesho litakalofanyika jijini Dar es Salaam leo, kushoto ni mwandaaji wa onyesho hilo, Edward Lusala. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Fally Ipupa kukiwasha Dar leo*

**Na Faustine Feliciane**

MSANII wa muziki wa dansi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo Fally Ipupa, amesema anajisikia fahari kufanya onyesho lake la kwanza jijini Dar es Salaam, baada ya kuzindua albamu yake mpya.

Fally Ipupa leo anatarajia kufanya onyesho jijini Dar es Salaam, ambapo ameahidi kutoa burudani ya kiwango cha juu kwa mashabiki wake na mashabiki wa muziki huo wa dansi.

"Ni mara ya kwanza nafanya onyesho baada ya kuzindua albamu yangu ni fahari kwangu kuona Tanzania ndio nchi ya kwanza kutembelea katika mpango wangu wa kuzunguka baadhi ya nchi za Afrika kutangaza alabamu yangu," alisema Ipupa.

Alisema kuwa yeye na wanamuziki wake wamejipanga kutoa burudani ya uhakika kwa mashabiki wake kwa kupiga kuanzia nyimbo zake za nyuma na nyimbo zilizopo, kwenye albamu yake mpya.

Kwa upande wake mratibu wa maonyesho ya mwanamuziki huu yatakayofanyika Dar es Salaam (leo) na jijini Mwanza siku ya Jumatano, kutoka kampuni ya Primetime promotion, Edward Lusala alisema mashabiki wa muziki huo, wajiandae kwa ajili ya burudani ya uhakika kutoka kwa msanii huyo.

"Tunashukuru sana ushirikiano kutoka kwa washirika wetu kampuni ya Startimes, ambao nao wamefanikisha kufanyika kwa onyesho hili kesho (leo) hapa Dar es Salaam na baadae Mwanza," alisema Edward.

Aidha, Mkurugenzi wa masoko wa Startimes, Tangji Yu, alisema wanafarijika kuwa sehemu ya waandaaji wa onyesho la mwanamuziki huyo, ambapo kampuni yake inafanya hivyo kuwapa burudani wateja wake.

Fally Ipupa ambaye amewahi kushirikiana na msanii wa Tanzania, Diamond Platinumz kwenye wimbo uliyopata umaarufu mkubwa ya 'Inama', leo anatarajia kukonga nyoyo za mashabiki wake, kwenye ukumbi wa Mlimani City, jijini Dar es Salaam.

## Waamuzi 70 kufanya mtihani

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

WAAMUZI 70 wanatarajia kufanya mtihani wa utimamu wa mwili (Copa test) kuelekea msimu mpya wa ligi Kuu Zazibar msimu wa 2021-2022.

Mtihani huo unatarajiwa kufanyika kesho Oktoba 10, 2021 majira ya saa 12:00 asubuhi katika Uwanja wa Amaan hapa Zanzibar.

Kati ya waamuzi hao, 40 wanatoka Unguja na ndiko watakaofanya mtihani huo Oktoba 10.

Akizungumza na gazeti hili Katibu wa Kamati ya Waamuzi (ZFF), Ali Juma alisema leo litafanyika zoezi la upimaji afya kwa waamuzi watakaofanya mtihani huo waliopo Unguja.

Alisema kati ya waamuzi hao 40, waamuzi wanne wanawake ndio watakaofanya mtihani huo.

Aidha, alisema Oktiba 16, zoezi hilo litahamia kisiwani Pemba, ambapo waamuzi 30, watafanya mtihani huo.

Alisema kwa Pemba litafanyika katika Uwanja wa Gombani majira ya saa 12:00 asubuhi, likitanguliwa na zoezi la upimaji afya.

## Mwinjuma awataka Kiba, Diamond

**Na Sabato Kasika**

MKONGWE wa muziki wa dansi Mwinjuma Muumini, amewataja wasanii wa sita wa muziki wa kizazi kipya, ambapo anawakubali na anatamani kufanya nao kazi kuwa ni Diamond, Nandy, Ally Kiba na Zuchu.

Amewataja wengine kuwa ni Jay Dee na Ruby na kufafanua, kuwa iwapo mmoja wao akitaka amshirikishe katika nyimbo, yupo tayari, kwa kuwa anawakubali na anapenda kazi za wasanii hao.

"Lakini mimi pia ninatamani kushirikisha mmoja wao katika nyimbo za bendi yangu ya Special, kwani hao ndiyo wasanii ninaowakubali hapa nchini kwenye muziki wa kizazi kipya," amesema Muumin.

Muumin amefafanua kuwa kutaja hao sita haimaanishi kwamba anadharau wengine, bali katika fani yoyote kila mtu anakuwa na watu wake maalum, ambao anawapenda kwa kuwa wanazidiana viwango.

"Tanzania ina wasanii wengi wa muziki wa dansi na hata kizazi kipya, lakini mimi nimetaja wale ambao ninawakubali, kwenye huo muziki wa kizazi na siyo kwamba wengine hawafai, bali ninavutiwa na hao," amesema.

Aidha, Muumin ameiomba serikali kuzitumia bendi za muziki wa dansi, kwenye shughuli na matukio yake kama inavyofanya kwa wasanii wa kada nyingine za burudani.

Amesema, lengo la kutoa ombi ni kutaka wanamuziki wa dansi nao wanufaike na shughuli hizo za kiserikali, kwa madai kwamba wameachwa nyuma hali ambayo inasababisha kuyumba kutokana na kukosa fedha.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### STERLING NA MKATABA

KLABU ya Manchester City ina nia ya kufungua mazungumzo ya mkataba mpya na Raheem Sterling, mwenye umri wa miaka 26 na hawataki kumuuza fowadi huyo wa England, ambaye amebakiza chini ya miaka miwili, kwenye mkataba wake. ***(Sun)***

### DEMBELE ALITAKIWA

BARCELONA imekuwa ikihusishwa sana na Raheem Sterling na Manchester City ingemtaka winga wa Ufaransa, Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 24, badala yake ikiwa mchezaji wao angehamia Camp Nou. ***(El Nacional)***

### ASENSIO ATAKIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL inazingatia uhamisho wa winga wa Real Madrid na Hispania, Marco Asensio, mwenye umri wa miaka 25, ambaye anaripotiwa hana furaha kule Bernabeu. ***(Mirror)***

### NEWCASTLE KUWA KUBWA

WAMILI wapya wa Newcastle wanalenga kuifanya klabu hiyo kuwa kubwa kama Manchester City na Paris St-Germain, ambayo pia wamiliki wake wanatoka Mashariki ya Kati. ***(Times)***

### WATAJWA NEWCASTLE

KOCHA wa zamani wa Chelsea, Frank Lampard na yule wa Rangers, Steven Gerrard wanazingatiwa kuchukua nafasi ya bosi wa Newcastle, Steve Bruce, ambaye amesema anatarajia kupoteza kazi yake. ***(Telegraph)***

### MCKENNIE ATAKIWA JUVE

JUVENTUS wameweka bei ya Pauni milioni 25.4, kwa ajili ya kiungo wa kati wa Marekani, Weston McKennie mwenye umri wa miaka 23, ambaye analengwa na Tottenham Hotspur. ***(Calcio Mercato)***

### ORIGI KUTUA BARCA

MSHAMBULIAJI wa Liverpool, Divock Origi ameripotiwa, kuwa atatua Barcelona Januari. Mkataba wa mshambuliaji huyo wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 26, unaisha mwishoni mwa msimu huu. ***(The Sun)***

### WINKS HUYO SPURS

KIUNGO wa kati, Harry Winks mwenye umri wa miaka 25 anaweza kuhamia Everton kutoka Tottenham Hotspur Januari, ili kupata wakati zaidi wa kucheza. ***(CaughtOffside)***

### CASTAGNE AGOMBEWA

JUVENTUS na Inter zinataka kumsajili beki wa pembeni wa Leicester mwenye umri wa miaka 25, Timothy Castagne. ***(Le Derniere Heure)***

### UMTITI ATAKIWA BARCELONA

AC Milan inataka kumsajili beki wa Ufaransa, Samuel Umtiti mwenye umri wa miaka 27, kutoka Barcelona Januari. ***(Calcio Mercato)***

## DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE ASEMA HANA TATIZO NA NEYMAR

●●● Amesema wakiwa mbele, kwenye ushambuliaji na wakishirikiana basi ana uhakika...

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe amesema alizungumza na mchezaji mwenzake Neymar katika klabu ya Paris St-Germain, kuhusiana na tamko la matusi alilotumia dhidi ya Mbrazil huyo katika mojawapo ya mechi zao, mwezi uliopita.

**Nyota huyo mwenye umri wa miaka 22 alisikika akisema "huyu makalio, hawezi kunipigia pasi" baada ya kutolewa uwanjani wakati wa mechi yao, dhidi ya Montpellier.**

"Ndio, ni kweli, nilisema hivyo. Haya ni mambo hutokea kila wakati katika soka," alisema Mbappe ambaye pia ni mshambuliaji wa timu ya taifa ya Ufaransa.

"Mara baada ya kugundua tamko hilo limegeuka kuwa kubwa, nilionggea nae."

PSG ilishinda 2-0 katika mechi ya Ligue 1, dhidi ya Montpellier kabla ya kuinyuka Manchester City mabao 2-0, katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya makundi.

Akizungumza katika mahojiano na L'Equipe, Mbappe alisema: "Tulishawahi kujibizana maneno kama hayo siku zilizopita na tutaendelea kufanya hivyo, kwa sababu tunataka kushinda, lakini hatufanyi hivyo kwa nia mbaya.

Hakuna chuki kabisa kwa sababu namheshimu kama mchezaji na mwanamume, pia napenda kile anachofanya."

Mbappe amesema kuwa yeye pamoja na Neymar Jr na Lionel Messi wakiwa mbele kwenye safu ya ushambuliaji, ikiwa watashirikiana basi ana uhakika kwamba watafanya vizuri kwa msimu huu wa 2021/22.

Kwa sasa timu ya PSG inatajwa kuwa ni timu yenye washambuliaji mahiri na uwezo mkubwa, ila wamekuwa wakishindwa kuwa na ushirikiano mzuri jambo ambalo lilifanya iweze kupata kichapo cha mabao 2-0, dhidi ya Rennes, kwenye mchezo wa Ligue 1, uliochezwa Oktoba 3.

MECHI KALI
HOME
AWAY
ETHIOPIA
3.87 | 2.76 | 2.11
SOUTH AFRICA

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 559



# MOURINHO: NATAKA MATAJI ROMA

**ROME,** Italia

JOSE Mourinho amesema anataka kubeba mataji akiwa na Roma, kwa sababu ana kikosi chenye uwezo wa kufanya hivyo.

Mourinho amerudi kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, akiwa na Roma kwa msimu huu 2021-22, baada ya kufukuzwa kule Tottenham, Aprili mwaka huu.

Roma wapo nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi, ikipitwa pointi sita na vinara Napoli, baada ya kushuka dimbani katika mechi saba msimu huu.

Giallorossihao hawajawahi kushinda taji la Ligi Kuu, Serie A, tangu mwaka 2001, huku wakiwa hawajabeba taji lolote tangu mwaka 2008, kitu ambacho Mourinho sasa anataka kubadili upepo.

"Ningependa kuwapa Roma taji, kwa sababu klabu inaishi kwa ajili ya mataji na uzuri ni kwamba molari hapa ipo juu zaidi," alisema kocha huyo wa zamani wa Chelsea, Inter, Real Madrid na Manchester United, akinukuliwa na jarida la Esquire magazine.

"Nimetambua kwamba, mashabiki hapa wana mapenzi ya kweli na Roma na kikubwa wanataka mataji.

"hata hivyo ushindi ni jambo lililokosekana hapa na kwa sasa mradi wetu ni kuhakikisha kwamba tunashinda."



# Lingard aitaka England

**LONDON,** England

JESSE Lingard anajua kwamba anahitaji kuwa kwenye klabu, ambayo atacheza mara kwa mara kuliko pale Manchester United wakati akitaka kuwa na nafasi kwenye kikosi cha timu ya taifa ya England.

Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer hajamtumia sana Lingard msimu huu, licha ya kuwa kwenye kiwango cha kuvutia kule West Ham alikokuwa ancheza kwa mkopo msimu uliopita.

Lingard alikataa kuzungumzia kuhusu majaliwa yake pale Old Trafford, huku mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Lakini kiungo huyo mshambuliaji, ambaye atafikisha umri wa miaka 30, wakati wa michuano ya kombe la Dunia mwaka 2022 nchini Qatar, anafahamu kwamba nafasi yake kwenye kikosi ch England, inaweza kuw kwenye tatizo kama hata pata nafasi ya kuchez mara kwa mara.

Baada ya kukosa m chuano ya Euro 202 Lingard hataki kuon anaosa tena michuan mikubwa.

"Kombe la Dunia ni nj ndefu, lakini unahita kucheza soka mara kw mara," alisema Lingar akiwaambia waandisl wa habari.

9,183,880

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 09/10/21 | 17:00 | Lugo vs Girona | 2.95 | 2.95 | 2.51 |
| 02. 09/10/21 | 17:00 | Hartlepool vs Northampton | 2.55 | 2.99 | 2.84 |
| 03. 09/10/21 | 17:00 | Bristol Rovers vs Carlisle | 2.55 | 3.09 | 2.75 |
| 04. 09/10/21 | 17:00 | Stevenage vs Exeter | 2.69 | 2.98 | 2.69 |
| 05. 09/10/21 | 17:00 | Sutton United vs Port Vale | 2.50 | 3.09 | 2.80 |
| 06. 09/10/21 | 17:00 | Barrow vs Leyton Orient | 2.55 | 3.14 | 2.70 |
| 07. 09/10/21 | 17:00 | Newport vs Bradford City | 2.79 | 3.19 | 2.45 |
| 08. 09/10/21 | 17:00 | Boreham Wood vs Dagenham and Redbridge | 2.49 | 3.22 | 2.68 |
| 09. 09/10/21 | 22:00 | Real Oviedo vs Sporting Gijon | 2.70 | 2.94 | 2.75 |
| 10. 10/10/21 | 08:00 | Matsumoto Yamaga vs Tochigi SC | 2.61 | 2.86 | 2.76 |
| 11. 10/10/21 | 15:00 | Real Sociedad B vs Ponferradina | 2.56 | 3.00 | 2.85 |
| 12. 10/10/21 | 19:15 | Alcorcon vs Burgos | 2.57 | 3.02 | 2.82 |
| 13. 10/10/21 | 22:00 | Fuenlabrada vs Leganes | 2.63 | 2.88 | 2.88 |


## MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMAMOSI - 09 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 4857 | VRI vs ASA Aarhus | 1.73 | 4.20 | 4.10 |
| 14:30 | 1143 | VSK Arhus vs Silkeborg Kfum | 1.98 | 3.62 | 3.19 |
| 14:30 | 1236 | KFUM Roskilde vs FC Roskilde | 4.46 | 4.27 | 1.57 |
| 15:00 | 1224 | Brabrand IF vs Naestved BK | 3.14 | 3.48 | 2.04 |
| 15:00 | 2754 | IFK Malmo vs Qviding Fif | 2.22 | 3.73 | 2.66 |
| 15:00 | 5262 | Aarhus Fremad vs HIK Hellerup | 1.91 | 3.50 | 3.50 |
| 15:00 | 5984 | Bayreuth vs Schweinfurt | 2.47 | 3.49 | 2.47 |
| 16:00 | 1239 | Tekstilshchik vs Tom Tomsk | 2.46 | 3.37 | 2.55 |
| 16:00 | 2210 | Blansko vs Frydek Mistek | 1.40 | 4.75 | 5.81 |
| 16:00 | 2436 | Guinea vs Sudan | 1.59 | 3.64 | 5.24 |
| 16:00 | 2952 | Ethiopia vs South Africa | 3.87 | 2.76 | 2.11 |
| 16:00 | 3006 | Kazakhstan vs Bosnia and Herzegovina | 4.51 | 3.56 | 1.79 |
| 16:00 | 4125 | Lithuania vs Bulgaria | 4.09 | 3.34 | 1.94 |
| 16:30 | 1956 | Aberystwyth Town vs Caernarfon Town | 2.75 | 3.53 | 2.23 |
| 16:30 | 3316 | Bala Town vs Cefn Druids | 1.08 | 9.12 | 17.47 |
| 16:30 | 3361 | Flint Town United vs Barry Town FC | 2.41 | 3.60 | 2.48 |
| 16:30 | 3545 | Admira Dornbirn vs FC Lauterach | 1.28 | 5.77 | 7.12 |
| 16:30 | 4487 | Newtown AFC vs Penybont | 2.29 | 3.54 | 2.67 |
| 17:00 | 1454 | First Vienna vs Bruck/Leitha | 1.29 | 5.21 | 7.72 |
| 17:00 | 2578 | Lugo vs Girona | 2.76 | 3.10 | 2.56 |
| 17:00 | 2700 | Ballymena Utd vs Crusaders Belfast | 3.24 | 3.78 | 1.92 |
| 17:00 | 2959 | Urozhay Krasnodar vs Neftekhimik | 3.78 | 3.25 | 1.91 |
| 17:00 | 3492 | Linfield Belfast vs Carrick Rangers | 1.32 | 5.02 | 7.15 |
| 17:00 | 5655 | Mirandes vs Eibar | 3.59 | 3.15 | 2.09 |
| 17:30 | 5690 | VVV Venlo vs Maastricht | 1.54 | 4.21 | 5.09 |
| 18:30 | 5522 | Audax Italiano vs CD Palestino | 1.94 | 3.29 | 3.62 |
| 19:00 | 1112 | Sweden vs Kosovo | 1.32 | 5.00 | 9.80 |
| 19:00 | 1114 | Azerbaijan vs Ireland | 3.70 | 3.05 | 2.16 |
| 19:00 | 3711 | Georgia vs Greece | 3.40 | 3.05 | 2.29 |
| 19:00 | 4839 | Ghana vs Zimbabwe | 1.22 | 5.24 | 11.64 |
| 19:00 | 5235 | Finland vs Ukraine | 3.31 | 3.11 | 2.29 |
| 19:00 | 5280 | Togo vs Congo | 2.55 | 2.84 | 2.84 |
| 19:00 | 5860 | Scotland vs Israel | 1.89 | 3.40 | 4.21 |
| 19:15 | 5452 | Almeria vs Las Palmas UD | 1.74 | 3.46 | 4.74 |
| 19:45 | 3455 | Emmen vs SBV Excelsior | 1.69 | 3.91 | 4.20 |
| 20:00 | 2051 | UD Extremadura vs Valladolid B | 2.07 | 3.24 | 3.29 |
| 21:45 | 1422 | Poland vs San Marino | 1.01 | 22.97 | 44.94 |
| 21:45 | 1591 | Faroe Island vs Austria | 12.02 | 5.81 | 1.24 |
| 21:45 | 1995 | Andorra vs England | 50.99 | 10.93 | 1.05 |
| 21:45 | 2669 | Switzerland vs Northern Ireland | 1.36 | 4.61 | 9.21 |
| 21:45 | 2896 | Hungary vs Albania | 2.06 | 3.15 | 3.90 |
| 21:45 | 3231 | Luxembourg vs Serbia | 7.03 | 4.62 | 1.43 |
| 21:45 | 3935 | Moldova vs Denmark | 34.96 | 9.59 | 1.08 |
| 22:00 | 3334 | Real Oviedo vs Sporting Gijon | 2.60 | 2.85 | 2.95 |
| 22:00 | 3594 | Guinea Bissau vs Morocco | 25.13 | 8.12 | 1.07 |
| 22:00 | 3776 | FC Eindhoven vs FC Oss | 1.97 | 3.61 | 3.32 |
| 22:00 | 3841 | Senegal vs Namibia | 1.24 | 4.75 | 12.61 |
| 22:15 | 3913 | Portugal vs Qatar | 1.22 | 6.61 | 11.02 |
| 22:30 | 2377 | Sport Recife vs Corinthians | 3.88 | 3.01 | 1.98 |
| 22:30 | 5473 | Atletico Mineiro vs Ceara CE | 1.37 | 4.35 | 7.34 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# POGBA: SIJUI MAJALIWA YANGU

**PARIS,** Ufaransa

PAUL Pogba bado hajajiandaa kutia saini mktaba mpya Manchester United, akisisitiza "ngoja tusubiri tuone" nini kitatokea baadae.


Kiungo huyo alionesha kiwango cha kuvutia, wakati Ufaransa ikitoka nyuma ya mabao 2-0 na kushinda 3-2, dhidi ya Ubelgiji kwenye nusu fainali ya Ligi ya mataifa ya Uefa katika uwanja wa Allianz pale Turin.

Pogba amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka United, akitajwa kutakiwa Juve na Real Madrid.

Taarifa za hivi karibuni zilibainisha kwamba, huwenda akaongeza mkataba wake na mashetani wekundu, ambapo kwa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu.

Ripoti hiyo ilisema kwamba, kusajiliwa kwa Cristiano Ronaldo na Jadon Sancho kumemfanya ashawishike kubakia klabu hapo.

Hata hivyo, akizungumza baada ya ushindi dhidi ya Ubelgiji, Pogba aliiambia Sport Mediaset: "Mara zote huwa nazungumza na wachezaji wenzangu wa zamani kama Paulo (Dybala).



# Matajiri wapya Newcastle wataka mataji

**LONDON,** England

WAMILIKI wapya wa klabu ya Newcastle United wamesema wanataka kuibadili na kuwa timu kubwa kama Manchester City na Paris Saint-Germain, baada ya kukamilisha kuinunua kwa Pauni milioni 305.

Mmiliki mwenza wa klabu hiyo, Amanda Staveley ameelezea matarajio ya ushirika wao unaosaidiwa na Mfuko wa Uwekezaji wa Umma wa Saudi Arabia (PIF).

Newcastle maarufu 'Magpies' sasa inakuwa klabu yenye wamiliki matajiri zaidi duniani.

Akizungumza na maelfu ya mashabiki waliokuwa wakishangilia makao makuu ya klabu hiyo pale St James' Park, Staveley alisema:"Tunataka kuona mataji. Laki mataji yanahitaji uwekezaji, muda, subira na ushirikiano."

Wamiliki hao wamependekeza Kocha wa sasa wa Leicester City, Brendan Rodgers kuwa mwalimu mpya wa Newcastle.

# Michezo

Jumamosi Oktoba 9, 2021

Nipashe




**Mbappe asema hana tatizo na Neymar** UKURASA 21




Naibu Spika wa Bunge la Tanzania, Dk. Tulia Ackson (katikati), akiwa katika picha ya pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa pili kushoto), Ofisa Biashara Mkuu wa GSM, Allan Chonjo (wa kwanza kushoto), Rais wa Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania, Phares Magesa (wa pili kulia) na Mwenyekiti wa CRDB Bank Foundation, Martin Warioba (wa kwanza kulia) wakati wa uzinduzi wa mashindano ya CRDB Bank Taifa Cup 2021, yanayotarajiwa kuanza Novemba 5, kwenye viwanja vya Chinangali, jijini Dodoma. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

# SIMBA YAJIFUNGIA KUISOMA GALAXY

## Yapata baadhi ya majina ya nyota wake, wana matarajio makubwa ya kwenda kufanya...

**Na Saada Akida**

HUKU baadhi ya wachezaji wa Simba wakiwa kwenye majukumu ya timu zao za taifa, kikosi kinaendelea na programu yake na benchi la ufundi likijifungia kwa ajili ya kuangalia video za wapinzani wao Jwaneng Galaxy FC.

**Mchezo wa hatua ya kwanza ya ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Jwaneng Galaxy utapigwa Oktoba 17 katika Uwanja wa Taifa wa Botswana, awali mchezo huo ulipangwa kucheza kati ya Oktoba 14 na 15 nchini humo.**

Benchi la ufundi la Simba linaloongozwa na Kocha Mkuu Didier Gomes akisaidiwa na Thierry Hitimana na Seleman Matola, tayari wameashaanza kupata baadhi ya majina ya nyota wa Jwaneng Galaxy ambao ni Bertrand ambaye ni usajili mpya kutoka Rwanda katika klabu ya Gasoline United na Gape Mohutsiwa.

Akizungumza na gazeti hili jijini, Kocha Msaidizi wa Simba, Hitimana alisema wameanza kuwafuatilia wapinzani wao licha ya kuangalia michezo ya nyuma kuanzia Februari ambapo walikuwa kwenye ligi na michuano hiyo ya hatua za awali. Alisema hatua hiyo ni baada ya kuchelewa kuanza kwa ligi ya Botswana hali iliyopelekea kukosa mechi nyingi za wapinzani hao.

"Tumeanza kuwafuatilia licha ya wenzetu ligi yao imechelewa kuanza, tunatumia mechi za hivi karibuni pamoja na taarifa za wachezaji wao ikiwemo usajili waliofanya kwa mchezaji kutoka Rwanda," alisema Kocha huyo.

Alisema wanatambua umuhimu wa mechi hiyo pamoja na ushindani wao na kuhakikisha kutumia vizuri ya kalenda ya FIFA na wachezaji waliobaki kufanya maandalizi ya mchezo wao dhidi ya Jwaneng Galaxy.

"Hawa waliobaki katika timu tutaanza nao mazoezi mepesi, kisha baada ya hapo tutakwenda kwenye mbinu ambayo na wale waliokuwa timu za taifa wataungana na wenzao katika hili," alisema.

"Baada ya hapo tutakuwa na muda mwingi wa awamu ya kuangalia mechi za Galaxy - zile za mashindano ya kwao na mchezo wa hatua ya kwanza waliocheza kisha kufahamu ubora na upungufu waliokuwa nayo," alisema kocha huyo.

Alisema kutokana na mipango waliyonayo kwa wachezaji na mbinu wanazofanya kipindi hiki, wana matarajio makubwa ya kwenda kufanya vizuri katika michezo yote miwili ya ugenini na nyumbani dhidi ya Watswana hao na kufuzu kucheza makundi.

# Stars ilikosa bahati- Poulsen

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa timu ya taifa ya Tanzania,Taifa Stars, Kim Poulsen, amesema walikosa bahati kwenye mechi ya juzi dhidi ya Benin, hali iliyosababisha wapoteze kwa bao 1-0 kwenye mechi ya Kundi J, kusaka tiketi ya kucheza Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar.

Stars imeondoka jana mchana kuelekea Benin na matumaini makubwa kufanya vizuri katika mchezo wa marudiano kufuzu Kombe la Dunia dhidi ya wenyeji wao hao.

Huku Kiungo wa Yanga, Zawadi Mauya, ameongezwa kwenye kikosi hicho akichukua nafasi ya Muzamir Yassi ambaye hatakuwepo kutokana na adhabu ya kadi mbili za njano.

Stars juzi ilipoteza kwa kukubali kichapo cha 1-0 kwa kupoteza pointi tatu muhimu, mchezo wa marudiano unatarajiwa kuchezwa Oktoba 10, 2021 nchini Benin ikiwa ni vita ya kusaka pointi tatu muhimu.

Taifa Stars iliondoka na Ndege ya Air Tanzania jana ikiwa na matumaini makubwa ya kuweza kupata ushindi licha ya kuwa mchezo huo utakuwa mgumu.

Wakati Kocha huyo akisema hayo, nahodha Mbwana Samata amewataka Watanzania kutokata tamaa kwani kuna mechi zingine tatu ambazo zinaweza kubadilisha matokeo ya msimamo wa kundi hilo.

Baada ya kumalizika mechi hiyo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Poulsen alisema walimiliki mpira kwa kipindi kirefu na hasa kipindi cha pili, lakini kwa bahati mbaya walipoteza nafasi nyingi.

"Tumecheza vizuri, lakini hatukutumia nafasi, hasa kipindi cha kwanza, Msuva alikosa nafasi kadhaa. Kipindi cha pili tuliwashambulia sana, lakini kwa bahati mbaya tukafungwa goli lililotokana na uwezo binafsi ya mchezaji mwenye jezi namba tisa Mounie (Steve), ambaye ana uzoefu. Alifunga bao zuri na Benin walitumia nafasi hiyo tu walioipata kipindi cha pili," alisema kocha huyo.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >